


WAKATI WA KANISA LA THIATIRA

 Sasa usiku wa leo tunaninii . . . Kabla tu hatujaingia kwenye wakati huu mkuu wa kanisa . . . Na—natumaini tu Bwana wetu ataimwaga Roho Yake juu yetu kuninii tu . . . na kutubariki tena. Nasi tunaweza tu kugusia mambo yaliyo muhimu sana sasa kwa sababu, katika tukio kuu la kuja, tungekuwa hapa juma zima. Na, loo, jana usiku tulikuwa na wakati mzuri sana!

² Vema, sasa kabla tu ya kuyasoma Maandiko, naomba tubadilishe tu ma—mahali petu kwa dakika chache na kusimama kwa ajili ya maombi:

³ Baba yetu wa Mbinguni mwenye rehema, tunakuja katika Jina litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, tukijua ya kwamba siku moja Wewe utakuja. Nasi tunajaribu kuitayarisha mioyo ya watu kuupokea huu ufunuo mkuu kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliye hai; hujafa, bali u hai milele; na unaishi katika Kanisa Lako kama shahidi wa Pentekoste, wa wakati ule mkuu hapo wakati wa kuburudishwa utakapokuja kutoka Uweponi mwa Bwana. Tuna furaha sana kuzifurahia nyakati hizo hapa chini baada ya miaka elfu moja mia tisa.

⁴ Na, Baba, kwa unyenyekevu tunaviinamisha vichwa vyetu kwa heshima ya hawa watu mashuhuri kote katika nyakati, hizo nyota ulizoshika mkononi Mwako, ambazo ulisema zilikuwa ni “malaika wa zile Nyakati za Kanisa,” wale wahudumu. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya Mtakatifu Paulo mashuhuri, wa Efeso. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya Ireneo, Ee Bwana, Ireneo yule mtumishi Wako hodari; na kwa ajili ya Mtakatifu Martin; na usiku wa leo kwa ajili ya Mtakatifu Columba. Bwana, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya watu hawa. Katikati ya Urumi mweusi, upagani ukiingia kanisani, walisimama kishujaa kwa ajili ya Ujumbe wa kipentekoste na baraka zake, kunena kwa lugha, na—na ishara kuu na maajabu, kuwaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu.

⁵ Wengi wao, Bwana, waliraruliwa vipande, wakauawa, wakalishwa simba; mambo makuu yalitukia. Dunia imeloweshwa damu ya wenye haki. Na, Baba, damu yao inalia leo hii dhidi ya kanisa hilo oву, la zinaa. Nawe ulisema, siku moja wakati ulipomwaga . . . “Malaika alipomwaga kitasa chake juu yake, na da—damu ya kila mfiia imani ilipatikana ndani yake.”

⁶ Bwana, tusaidie kuwa . . . kuwa tayari kusimama sasa, kwa kuwa wakati unakwisha. Tunapomwona mnyama huyu mwenye

pembe mbili akiinuka kutoka ardhini, sio kutoka kwa umati na wingi wa watu, “Akiwa na pembe kama mwana-kondoo, lakini akazungumza kama joka.” Tunaamini ya kwamba saa hiyo imekaribia sasa, Baba, wakati makanisa haya yanaungana pamoja, “Yakifanya sanamu ya mnyama”; na itakuwa mbaya sana kwa kundi hilo, Bwana, ambalo halitajiunga. Kule kususiwa kwenyewe kutakuja, lakini katika saa hiyo Wewe uliahidi kulichukua Kanisa Lako. Tusaidie, Bwana.

⁷ Kabla tone moja la maji halijaanguka, Nuhu alikuwa ndani ya safina. Kabla moto haujaipiga Sodoma, Lutu alikuwa ameondoka. Baba, tunaamini, kabla nguvu za atomiki kuilipua dunia hii vipande-vipande, Kanisa litakuwa limeondoka. Tuna furaha sana, Bwana. Na, tunajua ya kwamba mabomu yananing’inia kwenye mabanda, usiku wa leo.

⁸ Nasi tunaweza kuangalia kuelekea Mbinguni na kumwona Mwana wa Adamu akiinuka kutoka kwenye Kiti Chake cha Enzi aanze kuelekea duniani kwa ajili ya Unyakuo wa Kanisa Lake, na kujua ya kwamba miguu Yake ya thamani haitaigusa dunia hii yenye dhambi wakati huo; kwa kuwa kama vile Rebeka alivyopanda ngamia na kushuka kwenye ngamia, papo hapo kati ya nyumba ya Ibrahimu, huko kondeni alikutana na bibi-arusi wake. Ee Mungu, nalo Kanisa litakutana na Bibi-arusi wetu hewani, “Kwa maana sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia au kuwazuia hao waliokwisha kulala mauti. Parapanda ya Mungu italia, wafu katika Kristo watafufuka kwanza, nasi tutatwaliwa juu pamoja nao kumlaki Bwana (kondeni) hewani, na tuwe pamoja na Yeye milele.”

⁹ Loo, tusaidie, usiku wa leo, Bwana. Tupe utamu wa Roho zetu, na utuondolee chuki yote na kutokujali, na tuyeyushwe sana kwa Roho Mtakatifu. Jalia Malaika wa Mungu atawale usiku wa leo.

¹⁰ Bwana, sijui la kuwaambia watu hawa. Sasa, nimeandika historia na kadhalika za yale uliyofanya, bali inahitaji Wewe kuyafasiri mambo ya usoni, kwa hiyo naomba ya kwamba utatujalia katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹¹ Sasa hebu tufungue sasa kwenye Kitabu cha Ufunuo. Na usiku wa leo tuko kwenye wakati wa kanisa la . . . Wakati wa nne wa kanisa, Thiatira, wakati mkuu wa kanisa unaojulikana kama Wakati wa Giza. Wakati huu wa kanisa unaanza kwenye mwaka wa 606 kisha ukaisha kwenye mwaka wa 1520. Mimi . . . Yote ambayo ningeweza kufanya, ni kuuchagua. Wanachuoni wengi wanamchukua—wanamchukua Mtakatifu Patrick kuwa ndiye nyota ama ninii . . . kila . . .

¹² *Nyota saba* zilikuwa “malaika saba” wa zile Nyakati Saba za Kanisa. Tunajua kesho usiku, pasipo na tashwishi, Luther; na halafu Wesley. Hatujui huyu nyota wa kanisa la Laodikia atakuwa ni nani. Ni . . . Tuko kwenye huo wakati sasa, umekuwa

tangu mwaka wa 1906 mwanzoni mwa Pentekoste. Lakini kutakuwako na malaika atakayeinuka ambaye atayaangamiza mafundisho yote ya sharti, aliweke Kanisa tayari kwa ajili ya kwenda Nyumbani. Sasa, bwana fulani wa—wa . . . katika Roho, atakayeinuka pamoja na ishara na maajabu. Sasa, ninaomba ya kwamba Mungu atatusaidia kujua jambo hili.

¹³ Katika kumchagua huyu, tukiangalia kote, Mtakatifu Patrick alikuwa ni jamaa hodari. Na tukichukua baadhi ya maandishi ya kale, Mtakatifu Patrick hakuwa Mkatoliki. Alilipinga kanisa Katoliki. Na katika wakati wa yale Matengenezo, mafundisho hayo ya sharti waliyokuwa nayo yalichimbuliwa, na kuthibitishwa ya kwamba Mtakatifu Patrick alilipinga kanisa Katoliki. Hiyo . . . Mtakatifu Patrick alikuwa zaidi sana kama mtu wa kimadhehebu, alikuwa na shule yake mwenyewe. Yeye kwanza . . . wakati aliposhikwa mateka ufukoni mwa bahari, yeye, na dada zake wadogo wawili ambao hakupata kusikia habari zao tena. Walichukuliwa, labda wakapelekwa Rumi na kuuzwa kama watumwa. Yeye alichukuliwa pia na kuuzwa kama mtumwa na akapewa kazi ya kuchunga nguruwe.

¹⁴ Alifunza mbwa ku—kuwalinda nguruwe wake, na kadhalika; nao wangukuja kwa sauti mbalimbali na kadhalika ambazo angewapa hao mbwa. Na hatimaye hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kuepukia, chini ya mashua, wakati hao mbwa walimfunika mpaka akafika huko baharini. Baadaye akaja mahali pake pa kupendeza, Ayalandi, na kuwapata baba na mama yake wangali hai. Naye Mtakatifu Patrick alikuwa m—mpwa wake shujaa Mtakatifu Martin.

¹⁵ Ambaye, alikuwa ni mmoja wa watu hodari sana tuliopata kuwa nao katika mlolongo wa watu tangu Yesu Kristo, alikuwa ni Mtakatifu Martin. Makanisa yake yote yalijazwa na Roho Mtakatifu, wote walinena kwa lugha, walikuwa na ishara na maajabu, na miujiza, kila namna tu ya miujiza ikitendeka. Yeye aliidumisha Imani ya kipentekoste miongoni mwa wakati huo wa kanisa ambao ulikuwa ukifunga ndoa na Ukatoliki; upagani na Unikolai ukifunga ndoa pamoja, wakiunda dhehebu. Na kufanya U—Unikolai . . . Ambao sisi tunawaita *Niko*, maana yake “kushinda.” “Kushinda ama kuwapindua washirika,” na kumwondoa Roho Mtakatifu kutoka kwenye kusanyiko, na “kasisi pokee ndiye mtakatifu, huyo mtu tu.” Mnaona? Kisha wanaishi vyovyote watakavyo, nadhani, na mradi tu unakiri kwa kasisi. Basi wao . . .

¹⁶ Tuliona jana usiku, ya kwamba—ya kwamba waliwaweka, ya kwamba Konstantino alimweka askofu wa kwanza, na kuliweka . . . akawapa majumba haya, kama vile tulivyowapa tarehe na kadhalika ambazo mmeziandika. Na halafu walikuwa na kipindi cha sherehe kuu na karamu kule, ambacho kilikuwa ni tarehe 21 Desemba, siku iliyo fupi kuliko zote katika mwaka. Ndipo wakaingiza basi uzushi huu, kuwa, kwamba Yeye

alikuwa ni “siku ya jua.” Mnaona, si—siku ya kuzaliwa kwa jua, waliamisha kuzaliwa kwa Yesu Kristo kutoka Aprili hadi Desemba 25.

17 Desemba 25. Kote katika siku hizo tano ndiko Warumi walikuwa na sherehe zao kubwa, zile sarakasi, na kadhalika, na hapo ndipo walikuwa na karamu hii kuu ya kipagani. Nao wakamweka mtu huyu kama mungu mwenyewe pale juu, na kumvika na kila kitu. Nao wakawa na mungu wao pamoja nao. Na ninii. . . Hapo ndipo watu wa baada ya utawala wa miaka elfu walipoibuka, papo hapo, maana walidhani kanisa lilikuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu papo hapo. Mnaona, maana walikuwa ni tajiri, hawakuwa na haja na kitu, taifa na kanisa wote pamoja. “Utawala wa Miaka Elfu unaendelea,” lingali ni fundisho la Katoliki hata leo hii. Mnaona? Sasa, “ule Utawala wa miaka Elfu unaendelea,” kwa kuwa tunajua ya kwamba huo ni uongo. Ule Utawala wa Miaka Elfu: Kuja kwa Kristo Mara ya Pili kunauleta huo Utawala wa Miaka Elfu. Hiyo ni kweli.

Dunia inaugua, ikililia ile siku ya kufunguliwa kutamu,

Hapo Bwana wetu atakaporudi duniani tena.

18 Sasa, mtakatifu huyu mashuhuri hapa alikuwa ni Columba. Alikuwa ni mtu hodari wa Mungu.

19 Sasa, ninayo historia yake imeandikwa hapa. Kwanza, wakati wa nne wa kanisa, *Thiatura*, unamaanisha “zembe, kutokuwa mwangalifu,” ama “utusitusi.” Mnaona? Ulikuwa tu ni wakati haramu kutoka mwaka 606 hadi 1500.

20 Nyota ilikuwa ni Columba, kutoka Ayalandi na Uskoti, ambaye alikuwa ni mpwa wake Mtakatifu Martin; naye aliishi yapata miaka sitini baada ya Mtakatifu Patrick, na kwa hiyo huduma yake ilianza yapata miaka sitini baada ya Mtakatifu Patrick. Ninii yake. . .

21 Kamwe hakukubaliana na mafundisho ya Kirumi. Alikuwa ni mtu hodari wa imani. Aliyakataa mafundisho ya Kirumi; kamwe hakwenda Rumi, na aliukataa kabisa. Ni, nisingeweza kuona mahali walipomfanya mtakatifu. Kama walivyomfanya Mtakatifu Martin na hao wengine, hawakumfanya mtakatifu yeye na Ireneo kwa sababu walikuwa wangali katika Kanisa lile lililokuwa na ishara na maajabu ya Pentekoste, bali waliamini. Kamwe hakuchukua mafundisho ya Kirumi, kwenye mafundisho yao. Yeye alichukua mafundisho ya Biblia kama mama yake mtawala, dada ya Mtakatifu Martin, wala kamwe hakuyachukua mafundisho ya Kirumi wakati wowote. Alifundisha ya kwamba ishara za Marko 16 zinapaswa kumfuata kila mwaminio. Amina! Mimi. . . Huyu ndiye aina ya jamaa nimpandaye; anayeamini. Naam, bwana.

22 A—aliisikia Sauti dhahiri ya Mungu ikiita. Hiyo ni ishara nyingine nzuri kwake, mnaona. Basi hakuna kitu kingaliweza

kumkomesha baada ya hayo, aliondoka, uh-hum, uh-huh, alikuwa njiani wakati alipoisikia Sauti dhahiri ya Mungu.

²³ Mwijiza mmoja . . . ninayo mingi niliyoa- . . . hapa chini, bali tutachukua tu huu. Mwijiza mmoja ulikuwa kwamba wakati alikuwa ameenda kwenye mji fulani ambao Bwana alikuwa amemtuma, nao huo mji haukutaka kumpokea, kwa hiyo wakatoka na kujaribu kuninii . . . wakawachukua wanamuziki, na kadhalika, na kufunga milango na kujaribu kumhanikiza kwa kucheza, hao wanamuziki. Ndipo akaanza kuhubiri, ndipo ikawahanikiza wanamuziki nayo malango yakafunguka, akaingia ndani, akahubiri kwa vyovyote vile. Kundi lote likaongoka.

²⁴ Huu hapa mwingine mdogo ningetaka kidogo kuuzungumzia. Aliingia mjini. Miji yao ilikuwa imezingirwa na kuta siku hizo, hakika. Kwa hiyo akaenda kwenye mji huo, nao wakamfukuza. Alikuwa akiondoka, naye mtoto wa chifu akawa mahututi, nao wakamtuma mtu barabarani kumfuatilia huyo mtakatifu mwema. Alirudi na kujilaza kumkingama mvulana huyo aliyekuwa akifa, naye akafufuka.

²⁵ Kanisa lake lilijazwa Roho Mtakatifu, asingevumilia chochote pungufu, kwa kuwa kila mshirika wa kanisa lake hana budi kujazwa na Roho Mtakatifu. Naye aliupinga na kuuchukua sana ukasisi wa Rumi. Ninaamini alikuwa ndiye nyota ya wakati huo. Alikuwa akifanya nini? Pamoja na kunena kwa lugha, ubatizo katika Jina la Bwana Yesu, wakitekeleza mambo yale yale waliyoanza. Kama Mungu hana kikomo, na hivyo ndivyo alivyoliweka Kanisa Lake hapo mwanzo, halina budi kubaki vivyo hivyo, nalo (hata katika uchache) kote kote; karibu lilibanwa likaisha *hapa*, likarudi tena kupitia Luther.

²⁶ Sasa, tunataka kuanza sasa, tuone kama tunaweza kuanza kuvimalizia baadhi ya vifungu hivi sasa, kwenye . . . tutaanzia kwenye kifungu cha 18:

. . . *kwa malaika wa kanisa la Thiatira andika; . . .*

²⁷ Mliona hizi—hizi hotuba? Jumbe hizi zimeandikiwa malaika, ama mhudumu anayeibeba Nuru ya wakati huo wa kanisa. Mnaona? Sasa, jana usiku tuliona, katika kumaliza kwa wakati huu mwingine wa kanisa la—la Pergamo, ya kwamba malaika wa kanisa (katika kushinda kwa wakati huu wa kanisa) angepokea jiwe. Na katika jiwe hili . . .

²⁸ Sasa, tumelichukua hilo “jiwe” na kulionyesha kwa mfano, linamaanisha “mwamba.” Ni kitu gani? Malaika angekuwa ni mtu kama Petro, aliyeitwa “jiwe.”

²⁹ Angalia kwamba jina lako lina uhusiano na maisha yako. Sasa, siwezi kuingilia hilo sana, maana ibilisi ana numerolojia ya uongo; tunajua hilo; inawafanya watu kuanza *kuhisi*, na kadhalika namna hiyo, ambalo huingia katika ibada ya mizimu.

Na ibada ya mizimu ni ya ibilisi. Tunajua hilo. Na hivyo ndivyo, inavyowapasa kuwa waangalifu. Kama wao. . .

³⁰ Sababu ya wao kumwita Yesu “Beelizebuli,” “ibilisi,” kwa sababu, mnaona, angeweza kuyatambua mawazo ya moyoni mwao. Mnaona, bali Yeye alikuwa ni Neno la Mungu. Nayu Waebrania 4 ilisema, “Neno la Mungu, ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata huyatambua mawazo na makusudi ya moyo, nia.” Mnaona? Kwa hiyo, Yeye alikuwa Neno, Yeye ni Neno lililo hai, nalo Neno lililo hai huingia ndani yetu na halafu linakuwa na matokeo yale yale kwetu. Mnaona, yale yale, kwa sababu ni Neno lile lile. Mnaona, ni jambo lile lile miongoni mwetu. Na hiyo ndiyo njia. Na wakati mwingine wale wasio kwenye kikundi hicho hunena kwa lugha, na mwingine anafasiri. Ni kitu gani? Neno lililofanyika mwili tena miongoni mwetu.

³¹ Halafu basi, tunaona basi ya kwamba malaika huyu angepokea. . . malaika wa wakati wa kanisa aliyepokea lile “jiwe.” Lilikuwa ni jiwe *jeupe*, haimanishi haki yake mwenyewe, lakini “haki ya Mungu Mwenyewe.”

³² Na katika jiwe hili kulikuwako na “jina,” jina ambalo hakuna alijuaye ila yule aliyelipokea mwenyewe. Alilijua, bali hakuna mwingine angeweza kulijua ila yeye. Kwa hiyo mnapowasikia jamaa hawa wakijipendekeza kwenu, wakisema yao; hao ni “Yohana,” hao ni “Paulo,” hao ni “Mariamu,” hao ni “*huyu*,” “*yule*,” ama yule “*mwingine*.” Usiamini hilo, maana kama ni kweli, asingesema chochote kulihusu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hana budi kutolisema. Alilijua. Hakuna aliyelijua ila yeye mwenyewe, bali alijua kwa sababu kila mshindi mkamilifu hupokea jina jipya kwa—kwa—kwa njia hiyo.

³³ Mliona ya kwamba Ibrahimu aliitwa Abram, bali hapo Mungu alipoanza kumtumia, Yeye alilibadilisha jina lake likawa “Ibrahimu.” S-a-r-a alikuwa Sarai, bali Mungu alipotaka kumtumia, Yeye alibadilisha jina lake likawa S-a-r-a: Sara, “binti mfalme.” Hivi mnajua ya kwamba Yakobo. . .? Yakobo alikuwa “mchukua mahali pa mwingine.” Esau maana yake ni “mwekundu,” mwenye nywele nyingi na mwekundu; mwenye nywele nyekundu, na mwekundu kila mahali, ni Esau. Sasa, basi Yakobo alikuwa “mchukua mahali pa mwingine.” Na *mchukua mahali pa mwingine* ni “mdanganyifu.” Hivi Esau hakusema, “Si jina lake linaitwa Yakobo, ‘mchukua mahali pa mwingine’?” Lakini aliposhindana mwereka na Bwana usiku kucha, naye akashinda, na akabarikiwa, Mungu alibadilisha jina lake; Yakobo likawa *Israeli*, “mtawala pamoja na Mungu.” Paulo aliitwa *Sauli* mpaka alipokutana na Roho Mtakatifu katika umbo la Nuru iliyomwangazia, jina lake likabadilishwa kutoka Sauli likawa “Paulo.” Simoni, alipokutana na Yesu, Yeye alibadilisha jina lake likawa “Petro.” Hiyo. . .

³⁴ Na wakati Yesu aliposhinda, Jina Lake lilibadilishwa. Naye angelifunua Jina hilo, “Yeye ambaye angekuwa pamoja Naye, ashinde jinsi Yeye alivyoshinda, alipokea jina jipya; nami nitalifunua Jina Langu jipya kwake.” Mnaona? Na kila ashindaye, ninamaanisha, miongoni mwa watu kama hao: hao viongozi na kadhalika. Sasa, wana wote wa Israeli hawakubadilishiwa majina yao, hakika. Hiyo ni kweli. Lakini hao viongozi wakuu, waliposhinda, walikuwa wamepokea jina jipya. Mnaona jinsi linavyoingiana vizuri? Kikamilifu kabisa.

³⁵ Na sasa tunaona ya kwamba Yeye pia ana “mana iliyofichwa.” Sasa, mana iliyofichwa inafananishwa na mkate wa wonyesho. Mkate wa wonyesho ulikuwa wa makuhani pekee. Hiyo ni kweli. Mkate wa wonyesho ulikuwa tu ni wa kuhani. Nao. . . Ulikuwa ni kitu maalum kilichotengenezwa kwa ajili ya kuhani, hiyo ni kusema, viongozi; na mtu huyu alishinda. Kusanyiko lote lilipata mana, bali yeye alipata *mana iliyofichwa* (maalum), ama “*ufunuo maalum*,” loo, kwamba Yesu alikuwa ni nani, na kilichomhusu Yeye, yote kumhusu Yeye. Mnaona, alipata ufunuo huo kama alikuwa ameshinda, kwa malaika. “Shikilia sana, kwa kuwa yeye ambaye. . .” Yeye alikuwa ameshinda. Yaliandikiwa *malaika* wa kanisa. Mnaona?

³⁶ Sasa tunaona basi, usiku wa leo, tunaanzia:

. . . kwa malaika wa kanisa la *Thiatira*, andika; Haya ndiyo asemayo Mwana wa Mungu, yeye aliye na. . . macho. . . kama miali ya moto, na miguu yake. . . mfano wa shaba iliyosuguliwa sana;

³⁷ Sasa, tulipomwona kwenye ule wa kwanza, Wakati wa Efeso, ama katika mwanzo wa Ufunuo, tulimwona katika utu Wake uliotukuka wenye sehemu saba. “Nywele. . .” Tunaona ya kwamba Yohana alimwona katika siku ya Bwana.

³⁸ Anapokuja sasa, Yeye ni Kuhani. Wakati alipokuwa hapa duniani, alikuwa ni Nabii, Nabii wa Mungu. Sasa aliichukua Damu Yake Mwenyewe akaenda mbele za Baba, ambalo linamfanya Yeye Kuhani. Atakaporudi atakuwa Mfalme. Nabii, Kuhani, na Mfalme. Yeye alikuwa ni Nabii wa Mungu, alikuwa Tai. Alikuwa Kuhani wa Mungu, alikuwa Mwana-Kondoo. Atakaporudi, atakuwa Simba, Mfalme, (kabila la Yuda) kutawala.

³⁹ Lakini kati ya kazi Yake ya Kikuhani, wakati madhabahu yatakapoachwa, basi tunamwona amesimama pale. Naye Yohana alisema alikuwa katika Roho “siku ya Bwana”; sio siku ya saba, sio Jumapili, hayo yote ni makosa. Tuliona hilo, tukatafuta kote katika Maandiko, ilikuwa ni siku ya Bwana. Hii ni siku ya mwanadamu. Kule kuja kwa Bwana kutakuwa siku Yake.

40 Nasi tunamwona katika siku ya Bwana. Basi, alipomwona Bwana, Yeye alikuwa na “nywele nyeupe kama theluji.” Nasi tunajua kwamba hiyo inawakilisha hakimu.

41 Jambo lingine, Yeye hakuwa ni Kuhani wakati huo, maana Kuhani alikuwa amefungwa sehemu ya katikati, inamaanisha *utumishi*. Lakini Yeye alikuwa amejifunga matitini, *hapa* juu, ambalo lilimaanisha kwamba alikuwa ni *Hakimu*. Amina! Nasi tulimwona akitembea katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu.

42 Na sasa tulirejea nyuma kwenye yule “Mzee wa Siku,” akiwa *mweupe* kwenye ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi wakati Danieli alipomwona, “Akija kwa yule Mzee wa Siku ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama theluji.”

43 Sasa, “nyeupe.” Wale mahakimu wa kale wa Uingereza kote katika miaka, walikuwa, walipoenda kwenye kiti cha hukumu wangevaa wigi kubwa jeupe, wigi jeupe kama theluji, kwa sababu walikuwa ni mahakimu. Naye Yohana alimwona katika siku ya Bwana, wakati akiwa ni Hakimu. Amina!

44 Sasa tunaona ya kwamba “Alikuwa na macho kama miali ya moto.” Hayo macho wakati huo yalikuwa kama miali ya moto. . . Wakati mmoja hayo macho yalififia kwa machozi ya kibinadamu. Yangeweza kusimama na kumlilia mtu anayekufa, huku akijua katika dakika zingine tano ataishi tena; ila tu ni huruma ya kibinadamu. Lakini nyuma ya hayo kulikuwako na nguvu nyingi sana hata angeweza kuangalia moja kwa moja katika maisha ya mwanadamu na kumwambia alikuwa ni nani na yote kumhusu. Kwa sababu yalikuwa sasa yakija katika uakisi huu kama moto. Macho yanayoweza kuangalia huku na huku duniani, na kuona kila kitu kinachoendelea. Utasimama wapi katika Siku ya Hukumu? Dhambi zako zitakuwa wazi mbele Zake.

45 Nanyi mnaona alikuwa, “Kutoka kinywani Mwake, u— upanga mkali wenye makali kuwili,” ambao tuliona ulikuwa ni *Neno*.

46 Tuliona miguu Yake ilikuwa “shaba iliyosuguliwa sana,” na kadhalika, ambayo ilimaanisha “msingi Wake.” Anakanyaga mvinyo ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na kukanyaga-kanyaga na kujitwika dhambi, na kutoka, na kumfurahisha Mungu. Hiyo ni kweli. Nao msingi Wake ndio msingi wetu:

Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara,
nasimama; (alisema Eddie Perronet.)

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.
(Hiyo ni kweli.)

47 Sasa tunaona hapa, kila wakati anapokutana na wakati wa kanisa, Yeye anamzungumzia kama mmoja wa Majina Yake ya Kiungu. Sasa tunaona huko nyuma, wa kwanza katika funuo zote ni Uungu (Uungu Mkuu) wa Yesu Kristo: “Mimi Ndimi

aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Mimi ni wa kwanza, na wa mwisho, Mwenyezi Mungu.” Mnaona, ule ufunuo wa kwanza. Yohana aligeuka aone ni nani aliyekuwa akisema naye. Jambo la kwanza, alimwandikia kwenye . . .

⁴⁸ Mfalme yeyote, anapozungumziwa, hu—hu—husema yeye ni nani; mtu yeyote. “Mimi ni *Fulani-wa-fulani* ninapozungumza nanyi, hamnijui mimi. Mimi ni William Branham, Mimi ni *John Doe*,” yeyote yule.

⁴⁹ Alisema, “Mimi ni wa kwanza na wa mwisho; Yeye aliyekuwa hai na amekufa; na ni hai milele.” Loo, jamani! Ule Uungu. Hapa tunamwona katika utu Wake wenye sehemu saba wa hali Yake iliyotukuzwa. Katika kila wakati wa kanisa Yeye—Yeye huwakaribia katika moja ya huo uungu mbalimbali, nyingine ni ya hali hizo zilizotukuka.

⁵⁰ Sasa, usiku wa leo, Yeye anakuja pamoja na mwali wa moto. Anaangalia chini katika Laodikia . . . ama chini katika Thiatira. Huu ndio wakati ambapo kanisa limeolewa na Ukatoliki na upagani, ama Unikolai na upagani umefunga ndoa na kuunda na kuzaa kanisa la kwanza, kanisa la kimadhehebu.

⁵¹ Naye Mungu alisema ya kwamba *matendo* ya Wanikolai (yaliyokuwa katika Efeso), huko kwenye ma—maskini kanisa la Pergamo yalifanyika “mafundisho,” na kasema yalikuwa ni “mafundisho ya Balaamu.” Naye Balaamu alikuwa ndiye aliyewafundisha Israeli kwenda kule na kufanya uasherati, ama walifanya uasherati na Moabu (ambao walikuwa wafuasi vuguvugu wa kanisa), ama kanisa la kawaida, lile dhehebu kuu. Nasi tunaona ya kwamba Mungu alisema, ya kwamba mafundisho ya Wanikolai ambayo yalikuwa ni . . . kuchukua ninii . . . kuweka mamlaka yote katika kanisa na kuliweka kando na kulifanya dhehebu, Yeye alisema, “Mnayachukia, nami nayachukia pia.” Anaendelea tu kusema, “Nayachukia! Nayachukia! Nayachukia!” Nayoyamefikia kilele chake *hapa*. Mnaona jinsi ambavyo kanisa lilibanwa sana, papa *hapa* mpaka likasalia kitu kidogo sana, na hilo ndilo kanisa tunalozungumzia sasa.

⁵² Sasa, katika siku hii ambayo ufunuo huu umekuja, ama uliokuwa kwa kanisa hili, ilikuwa ni siku ambayo Rumi ilikuwa imejengea juu ya yale mawe makubwa sana ya mahali pao, ya nyasi kavu na nyasi. Lakini Yeye anahutubia kanisa hili ambalo “Yeye angali ni miali ya moto ambayo inaangalia kupita kwenye wakati, wala msingi Wake sio nyasi kavu, magugu, lakini ni shaba imara, iliyojaribiwa kwenye tanuru inayowaka moto.” Msingi ni imara. Ninapenda hilo. Tunajua mahali tunaposimama.

⁵³ Vema:

Nayajua matendo yako, na upendo wako, na huduma yako, na imani, na subira yako, na matendo yako; tena

kwamba matendo yako ya mwisho—mwisho yamezidi yale ya kwanza.

54 Vema, kanisa linaonekana kuwa karibu limekatiliwa mbali kabisa, kupungua kidogo tu, nao walikuwa wameachana na ile mikutano mikubwa ya kiroho, na kidogo walikuwa wakiyategemea matendo. Mungu hataki tuyategemee matendo.

55 Hiyo ni i—ishara ya mpangilio. “Tutampelekea Binti Jones kuni kidogo. Kisha tuwapelekee *Fulani-wa-fulani*, watoto wao, nguo chache.” Na hilo ni sawa. Lakini, usitegemee hayo, usifanye hivyo. Ndugu, hayo—hayo—hayo ni matendo mazuri; raia mwema, mwadilifu atafanya hivyo. Lakini kinachohitajika kuwa Mkristo ni tukio la kuzaliwa mara ya pili, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Vema.

56 Walififia kabisa, waliishia kwa matendo badala ya upendo na imani, wakipata mengi zaidi na zaidi wakati wote likiendelea.

57 Vema:

Nayajua matendo yako, . . . najua imani yako, najua subira yako, na kadhalika . . .

58 Lakini sasa tutachukua kifungu cha 20, sikilizeni haya:

Lakini nina maneno machache juu yako, kwa kuwa unamridhia yule mwanamke Yezebeli, yeye ajiitaye nabii, kuwafundisha na . . . kuwashawishi watumishi wangu na kufanya uasherati, na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.

59 Sasa, “mwanamke.” Tuliona *mwanamke* aliwakilisha nini jana usiku? “Kanisa.” Sasa, sasa tunaona hapa kwamba waliitwa “Wanikolai,” “mafundisho ya Balaamu,” na sasa yamekuwa “Yezebeli.”

60 Sasa, “Yezebeli.” Kama mtaangalia, hii ni historia kuu. Sasa, kama mkitaka kuandika, anzieni katika Wafalme wa Kwanza, yapata . . . Wafalme wa Kwanza, yapata 16. Yezebeli hakuwa binti ya Ibrahimu; wala na kundi hili hapa, Rumi ya kipagani. Wanikolai walikuwa ni kundi la Wakristo baridi wa kawaida, ambao walikuwa wamejitenga na Wakristo halisi, “wakionekana hawana ile Imani.” Nao walitaka kulifanya kanisa kama chama, kama vile walicho nacho siku hizi; kama chama, hakuna Roho ndani yake hata kidogo; “Siku za miujiza zimepita. Hayo yote yalikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Tunao udugu.” Mwashu mzuri, Jamaa Mpweke, ama kitu chochote kama hicho hubuni huo. Na hiyo ni sawa, bali huo kamwe hautachukua mahali pa kuzaliwa upya katika Yesu Kristo, wokovu kwa nafsi, Ukweli huu.

61 Vema, huyu Yezebeli. Sasa alikuwa ni binti wa Ibrahimu, hiyo ni kweli, binti mfalme wa mwabudu sanamu. Wakati huo wakati familia ya kifalme, familia yake ya kifalme, walijulikana

sana kwa utiifu katili wa kinyama kwa Mabaali. Baba yake alikuwa ni kuhani wa sanamu ya A-s-t-a-r-t-e (sijui jinsi ya kulitamka, nililichukua tu katika historia). Ahabu alitumia mbinu zake kama Konstantino. Taifa hili lenye nguvu lilipakana na Israeli, kwa hiyo basi. . .

⁶² Konstantino alifanya nini jana usiku? Hakuwa ameongoka. Alikuwa ni mwanasiasa. Alikuwa akijaribu kufanya nini? Aliwachukua Wakristo, wakati walipomwambia wangeomba. . . (Na sasa pale, kumbukeni, yeye ana- . . . tunazungumza sasa juu ya Wanikolai). Naye akasema kama wangeomba, naye ashinde vita hivi, basi ange—angekuwa Mkristo. Aliota ndoto. Akapaka ngao zake rangi nyeupe, usiku huo, ya msalaba. Ambapo Mashujaa wa Columba walizaliwa, papo hapo kwenye wakati huo; sasa hapa ndipo wanapouchukua msimamo wao. Bali kamwe hakutenda kitu chochote kama Mkristo! Kwenye moja ya makanisa ya Wanikolai, linaloitwa Mt. Sophia, aliweka msalaba. Kama nilivyosema jana usiku, hilo ndilo jambo pekee alilopata kufanya lililosikika kwa chochote kile kana kwamba alikuwa wa kanisa, kadiri nilivyoweza kuokota kutoka kwenye kurasa zozote za historia; na wanachuoni wengine wengi husema jambo lilo hilo. Hatujui lolote juu ya wongofu wake, sasa. Lakini aliingilia kitu gani? Jambo alilotaka kufanya, alikuwa ameona karibu Rumi yote, sasa.

⁶³ Sasa angalia jambo hili, angalia mbinu hii. Pia angalia jinsi Biblia inavyolithibitisha, Mungu, mamia na mamia ya miaka kabla halijatukia. Naye Konstantino alitumia mbinu iyo hiyo, Mungu alisema hapa, ambayo Ahabu alitumia.

⁶⁴ Sasa, Konstantino aliona sehemu kubwa ya watu wake ilikuwa ni hawa Wanikolai, Wakristo. Baadhi yao waliitwa “wazushi,” hao ni Wapentekoste; walikuwa ni “wazushi na watakatifu wanaojibingirisha,” na chochote kile. Hapo ndipo ishara zenu halisi na maajabu yalipokuwa. Lakini kanisa la *kawaida* wakati huo lilikuwa likielekea kwenye umadhehebu. Yeye alifanya nini? Konstantino alifanya mbinu za ujanja. Anaondoka anaenda kule na kuwachukua marafiki zake wapagani, kisha anawachukua marafiki zake Wakristo, na kuyaunganisha makanisa pamoja, akaanzisha ninii—ninii. . . akaingiza upagani katika Ukristo. Ukristo na upagani ukafunga ndoa katika kanisa la Pergamo.

⁶⁵ Sasa, Yeye alisema nini hapa kwa jambo hili usiku wa leo? Jambo lile lile alilofanya Ahabu. Ahabu, kuimarisha ufalme wake, alimwoa Yezebeli, huyu mwanamke mwabudu sanamu; apate kuimarisha ufalme wake, apate kuingiza nguvu zaidi katika Israeli.

⁶⁶ Na hayo ndiyo makanisa yanajaribu. Mnaona mahali wanapojaribu kuifanya Biblia, waitoe mwaka ujao wa '62? Hiyoi ni Biblia itakayowafurahisha Wayahudi, itawafurahisha

Wakatoliki, na kuwafurahisha Waprotestanti. Loo, ndugu! Ninayo makala iliyokatwa kutoka gazetini. Sinayo usiku wa leo, mlinisikia nikiyasoma hivi majuzi usiku hata hivyo. Haya basi, mnaona.

⁶⁷ Loo, hayo mambo kujaribu kuongezeka! Wanavichukua vitu vitakatifu vya Mungu na kuvitapanya kwa njia yoyote, wapate kuongezea na kupata idadi kubwa ya wafuasi. Hivyo ndivyo kanisa limefanya. Liliwakubali watu ndani yake kwa misingi ya kupeana mikono, nao wakapata wahaini na kila kitu kingine, watu wasioongoka. Bali katika Mwili wa kweli wa Kristo, ambao si dhehebu, bali wa kisiri—Mwili wa kubuni wa Kristo, unaweza tu kuingia mle kwa njia moja, na hiyo ni kupitia kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kweli! Na ishara zile zile zilizowafikia hao mitume, zinalifikia Kanisa. Hiyo ni kweli kabisa!

⁶⁸ Sasa, haitulazimu kupatana na kusema, “Vema, tutaenda tukajiunge na Assemblies. Tutaenda tukajiunge na Waumoja. Tutaenda tukajiunge na *hili*, ama Baptisti, ama Methodisti.” Hebu tujiunge na Kristo! Tukae huru na mambo haya. Maana kila moja ya madhehebu hayo ni sawa, bali wa—wanachukua mafundisho yao na kadhalika, nawe inakubidi kwenda kuona kama msimamizi mkuu atakuruhusu uingie humo nchini na kufanya mkutano. Kama hufundishi jinsi hasa wanavyofanya, wanakufukuza, huwezi kudumu na Biblia. Mungu hawezi kufanya hivyo, Yeye analichukia. Mkristo mwingine yeyote aliyezaliwa mara ya pili angelichukia pia. Wengi wa hao watu huko nje wananinii kabisa... wanataka kufanya, wanataka kutumika, na wanataka ushirika. Bali huwezi kufanya jambo hilo, wangekufukuza. Vema, acha wakufukuze, endelea, mpate Roho Mtakatifu kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini, unaona, wa—wanataka kupata fundisho hilo—hilo la sharti. Wanataka kuwapata ninyi mlio na fedha nyingi. Wabaptisti walikuwa na msemu katika mwaka wa '44, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44.” Walipata nini?

⁶⁹ Kama tu vile yule mwinjilisti mashuhuri Billy Graham alivyosema, alipokuwa Louisville, “Nitaingia mjini...” Kasema, “Mtakatifu Paulo ataingia mjini, atampata mwongofu mmoja; akirudi mwaka ujao ame—amepata thelathini kutoka kwa huyo mmoja; wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu, kutoka kwa mwongofu huyo mmoja.” Akasema, “Mimi nitaingia mjini, niwaite elfu thelathini huku, nitarudi mwaka ujao na siwezi kupata thelathini.” Na yale aliyosema, a—alitoa tamshi zuri, bali hata hivyo siamini ndugu yetu wa thamani alikuwa sahihi. Alisema, “Enyi wahubiri wazembe.” Kasema, “Nitawapa majina yao na anwani, mnaketi mmeweka miguu yenu kwenye dawati na kuwaandikia barua badala ya kwenda, mkazungumze nao.”

⁷⁰ Ki—kidogo nilipendezwa naye kwa jambo hilo. Napenda mtu awe jinsi alivyo, sio mnaofiki; simama papo hapo na uwe jinsi

ulivyo. Nami napenda hilo. Ila ningetaka kusema, “Billy, ni nani aliyekuwa huko juu kumchukua huyo mwongofu wa Paulo? Jambo ni kwamba, Billy, kama ungeachana tu na kuwaacha waende kule nyuma na kupeana mikono, na kusimama, na kusema, ‘Naam, ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi,’ na kuacha akae pale mpaka afe na kuoza, na kuzaliwa mara ya pili na Roho Mtakatifu, yeye atawapata waongofu wanya.”

⁷¹ Ndugu, wewe ni. . . anawaka moto, huwezi kumzima. Yeye ni kama nyumba inayoteketea katika upepo mkali, kamwe huwezi kuuzima. Loo, anasambaza kila mahali, ndugu, mwongofu halisi wa Kristo, hawezi kutulia. Yeye ni ninii tu. . . yuko mbioni. Loo, nina furaha sana! Loo, jamani! Ubatizo wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu ambao huiwasha moto nafsi yako! Huwezi kutulia, upepo unakupulizia, upepo wa nguvu ukienda kasi utaendelea tu kukupulizia. Ndiyo sababu ninaendelea kuuongezea kuni, na kuzidi kuendelea. Naam, bwana! Haikumbidi mtu yeyote kumchukua mwongofu wa Paulo, Paulo aliwaingiza kwa kilindi vya kutosha ndani ya Kristo mpaka akaifia nafsi yake, akawa hai katika Kristo, *naye* akafanya yaliyosalia. Hiyo ni kweli! Hivyo ndivyo ilivyo.

⁷² Ndugu wa Kibaptisti ni sawa. Lakini milioni moja zaidi, inaleta faida gani? Unayo majina milioni moja zaidi. Vema, keti tu chini na uwafanye wengine kama unataka kuwaandika mle. Hilo ni sawa, lakini, ndugu, tunachohitaji ni majina kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, waliooshwa katika Damu, wakajazwa na Roho Mtakatifu, ishara na maajabu zikiwafuata.

⁷³ Tafuteni katika historia. Laiti nyote mngkipata kile cha Mabaraza ya Nikea na kuyasoma mambo hayo, muone jinsi hao wafia imani walivyoushikilia ule mwali wa moto wa pentekoste. Nitawaambia sasa, ndugu, ninyi Wabaptisti, Methodisti, na chochote mlichu, ile Nuru ya kweli halisi. . . sio dhehebu la Kipentekoste, sasa; bali Nuru ya kweli na halisi, ni Tukio la Kipentekoste. Chini. . . Nimekuwa siku kadha wa kadha sasa, historia hizo, nikazichambua katika zote ninazoweza kupata kila mahali, na ni ule mwali wa moto wa pentekoste uliodumu hai tangu Pentekoste hata wa leo. Naam, bwana! Umesukumwa nje.

⁷⁴ Baadhi yao husema, “Vema, lile kanisa kuu la Katoliki limeyastahimili mawimbi. Mbona, inathibitisha ya kwamba hilo ndilo Kanisa halisi.” Mbona, hilo si jambo la kigeni kwangu, huku taifa na kila kitu kikiwa nyuma yake, lingaliweza kudumu. Lakini kitu cha—kitu cha kushangaza, ni lile kundi dogo lililojiondoa, maskini ule uchache, waliofukuzwa, wakatupwa gerezani, wakakatwa kwa misumeno vipande-vipande. Walipataje kuishi? Kwa sababu Roho wa Mungu aliye hai anatenda kazi katika utu wao. Wala poto wote wa kuzimu

hawawezi kulishinda! “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Hicho hapo kile kitu halisi. Hicho ndicho kinachowapa Roho Mtakatifu hawa wahubiri wa Methodisti, na kadhalika, hapa. Mnaona, anawafanya kuamka, anakufanyia jambo fulani. Hatashindwa kamwe.

⁷⁵ Ahabu, yule mnafiki. Mnaona, anaenda kule, anasema, “Sasa, laiti ningaliweza kuwaunganisha sasa, na kulipata taifa hili kubwa. Na kama nikimwoa binti wa maskini jamaa yule kule chini, vema, hilo . . . tu—tutakuwa marafiki.” Alikuwa akifanya nini? Akiuza haki zake zenye za mzaliwa wa kwanza.

⁷⁶ Sasa, wakati kanisa hili la Kiprotestanti litakaporudi *kweli* na kuungana na kanisa Katoliki, litafanya jambo lile lile lililofanya huko nyuma. Ahabu aliishi kwenye siku ambayo . . .

⁷⁷ Imekuwa mara tatu. Alikuwa katika tukio la usiku wa manane wa safari ya Israeli, na *hapa* ukafikia usiku wa manane tena, nasi tunaufikia usiku wa manane tena *hapa*. Vizazi vitatu kabla ya hiki; waliingia *hapa* ndani, *hapa* ndani, na *hapa* ndani.

⁷⁸ Sasa, kama ukiangalia, Ahabu alimwoa Yezebeli kuwaimarisha watu wake. Hivyo ndivyo Konstantino alivyofanya hasa. Alianzisha kanisa kubwa mno, kisha akachukua madhabahu na kufanya marmar kubwa, akamvalisha mtu huyu, papa, akampandisha kule juu. Alikuwa ni mungu aliye hai, angeweza kusema nao, na—na kumwambia juu ya dhambi zake, basi hilo lililifurahisha kabisa maskini kanisa hilo vuguvugu, nao wakaondoka. Hakika! Jambo ndilo hilo! Vema, ila hilo halikumfurahisha mtu huyu aliyezaliwa mara ya pili, walipolichukua hilo na halafu kuingiza sherehe za kipagani za kukariri maombi. Walifanya nini? Walishusha Jupita, wakampandisha Petro. Wakashusha Venasi, wakampandisha Mariamu. Nalo likaingiza—likaingiza upagani katika matabaka ya Kikristo.

⁷⁹ Basi Ahabu alipomwoa Yezebeli, alifanya jambo lile lile tena. Aliingiza ibada za sanamu katika Israeli. Naye Yezebeli alifanya nini? Alimwua kila nabii aliyeweza kumshika. Hiyo ni kweli? Vivyo hivyo na mapapa pia. Kila Mkristo wa kweli waliyeweza kumshika, waliwaua.

⁸⁰ Bali kulikuwako na nyota ya wakati huo, maskini Eliya! Loo, naam, bwana! Yeye hakuogopa, kuwaambia habari zake. Naam, bwana! Yeye alikuwa ni nyota ya Mungu ya wakati *huo*. Ilifikia wakati mmoja akasema, “Bwana, ni mimi pekee nimesalia.”

⁸¹ Mungu alisema, “Sasa, ngoja kidogo, ngoja kidogo, ngoja kidogo, Eliya.” Uh-huh. “Tayari ninao mia saba waliofichwa huku na huku, huko. Mnaona? Hujui walipo. Wako huko nje, Mafarisayo, Masadukayo, Wabaptisti, Wamethodisti, na Wapresbiteri, bali nita—nitawatoa huko, wewe ngoja tu. Unaona? Ninao huko nje. Kuna ninii . . . hao ni—hao ni—hao

ni Wangu, nao bado hawawapigii Mabaali goti.” Lakini maskini Eliya alikuwa Sauti ya Mungu katika siku hiyo. Hakika alikuwa ni mfano wenyewe wa Sauti ya Mungu katika kule kuja kwa Kristo mara ya kwanza, na atakuwa ni mfano wa Sauti ya Mungu katika kuja kwa Kristo mara ya pili tena, kulingana na Maandiko.

⁸² Sasa, tunaona ya kwamba maskini Yezebeli huyu, wakati alipofika kule, alikuwa kweli anaenda kuangusha madhabahu yote ya Mungu na kujenga madhabahu yake mwenyewe. Naye aliwafanya Israeli kusujudu mbele ya sanamu. Hivyo ndivyo hasa Konstantino alivyofanya hapo alipoliunda kanisa Katoliki. Aliingiza upagani katika ka—kanisa la Kikristo, na kuwafanya Wakristo kusujudia sanamu. Huo ni wakati wa giza kabisa tena; wakati wa giza wa Israeli, wakati wa giza wa—wa kanisa; kusujudia sanamu. Basi Eliya alikuwa ndiye nyota katika siku zake.

⁸³ Naye akawafanya Israeli wote kuabudu Mabaali, vivyo hivyo na kanisa Katoliki huko Thiatira.

⁸⁴ Sasa, nawatakeni muone jambo lingine la kushangaza hapa, nilikuwa nikichukua historia yangu hapa. Yesu alisema ya kwamba lilikuwa . . . lilijiita nabii. “Huyo mwanamke Yezebeli, anayejiita (anajiita) nabii.” Sasa, mnaona, kanisa Katoliki haliwaruhusu watu wao kuisoma Biblia kwa sababu wanasema ya kwamba kasisi ndiye pekee anayeweza kulitabiri Neno hilo Kiungu.

⁸⁵ Vema, hiyo ndiyo fasiri ya kweli ya nabii. Nabii anayo fasiri ya Kiungu ya Neno la Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Mtu anawezaje kumwita mtu, mtu fulani, “nabii” kisha aseme, “wana ufunuo mbaya”? Lina maana tu kama uwana wa Milele tena, mnaona. Mnaona? Mnaona, ni—ni ninii. . . *Nabii* maana yake ni “mtabiri halisi, yule ambaye hujiliwa na Neno la Bwana, aliyejiliwa na ufunuo.” Neno *nabii* linamaanisha “mtabiri wa Neno la Kiungu.” Yesu alisema, “Akitokea miongoni mweni mtu ambaye ni wa kiroho ama nabii, mimi Bwana nitasema naye. Na kama asemalo likitimia, basi msikieni, niko pamoja naye. Kama halitimii, basi msimsikie.” Hivyo tu. Lilikuwa ni—lilikuwa ni Neno la Kiungu la Mungu, nalo Neno la Bwana liliwajia manabii.

⁸⁶ Sasa, walisema kwamba *kanisa* hili basi lilikuwa ni “nabii.” Sasa kumbukeni, limebadilika kutoka kwenye hili la Wanikolai sasa, limebadilika likawa ni “*mwanamke*.” Mnaliona? “Yezebeli.” Sasa, jana usiku ilikuwa ni “mafundisho ya Balaamu.” Mnaona, “fundisho la Wanikolai” na “fundisho la Balaamu.”

⁸⁷ Sasa, Balaamu alikuwa ndiye aliyefanya ukahaba na Israeli. Basi Wa—Wa—Wanikolai walifanya nini? Waliunda dhehebu. Basi waweke wote wawili pamoja nawe utapata *mwanamke*,

“kanisa.” Hakika! Ufunuo 17, “Yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi.” Mwanamke, kahaba. Yeye ni nini, ama yeye ni kahaba vipi? Anafanya uasherati, uasherati wa kiroho, kulifasiri Neno vibaya kwa watu. Uondokeeni huo ushupavu! Huo ni ushupavu kwelikweli. Hiyo ni kweli.

⁸⁸ Sasa, mnaona, anajiita nabii, “Sisi ndio! Sisi ndio lile baraza! Sisi ndio baraza la Laodikia tena, baraza la watu, nasi tumeamua *hivi*, na *hivi*, na *hivi*. Kwa hiyo tusikilizeni!” Lakini . . .

⁸⁹ Maskini yule—yule kasisi hapa juu kunihoji kuhusu Elizabeth Frazier, ama yule msichana wa Frazier. Kasema, “Ka—kadinali anataka kujua kama utaninii . . . ama askofu, kama ulimbatiza msichana huyu wa Frazier.” Kasema, “Anakuwa Mkatoliki.”

Nikasema, “Naam, ninaelewa hilo.”

Kasema, “Hivi—hivi ulimbatiza?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Kasema, “Ulimbatizaje?”

Nikasema, “Katika ubatizo wa Kikristo.” Uh—huh.

Akasema, “Vema, unamaanisha nini na hilo?”

Nikasema, “Ubatizo wa Kikristo, vile Biblia isemavyo. Kuna njia moja tu ya kubatiza katika ubatizo wa Kikristo. Kila mtu katika Biblia alibatizwa chini ya maji katika Jina la ‘Yesu Kristo.’”

⁹⁰ Akaandika hayo, akaanza kuandika namna hiyo. Kasema, “Unajua, kanisa Katoliki lilikuwa likifanya hivyo.”

Nikasema, “Lini?” Nikasema, “Ninazo historia zote za kale hapa ambazo ningeweza kupata, kutoka London na kokote kule.” Kusudi nipate kusoma wakati majira haya yatakapokaribia hivi karibuni, wakati jambo fulani litakapotukia. Hmm. Nikasema, “Na—nataka kujua ni wapi.” Ningeenda . . .

Akasema, “Loo,” akasema, “katika Biblia.”

Nikasema, “Unasema ya kwamba . . .?”

Akasema, “Yesu aliliunda kanisa Katoliki.”

Nikasema, “Je, Petro alikuwa ndiye papa wa kwanza, basi?”

Kasema, “Bila shaka kabisa.”

Nikasema, “Nilifikiri ‘kanisa lisingeweza kufanya kosa wala halibadiliki, na misa zote zilisemwa katika Kilatini zisije zikabadilika.’”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

⁹¹ Nikasema, “Vema, hakika mmebadilika sana tangu wakati huo.” Nikasema, “Ikiwa Biblia hiyo ni kitabu cha Katoliki, basi

mimi ni Mkatoliki wa mtindo wa kale.” Mnaona? Hiyo ni kweli. Nikasema, “Mimi ni Mkatoliki wa mtindo wa kale, basi.” Kisha nikasema, “Hakika lilikuwa na . . .”

Akasema, “Vema, sasa, mnaona, Biblia ni historia tu ya kanisa Katoliki.” Akasema, “Mungu yuko ndani ya kanisa Lake.”

Nikasema, “Mungu yuko katika Neno Lake.” Hiyo ni kweli.

⁹² “Neno Langu na liwe kweli, na neno la kila mwanadamu liwe uongo.” Na hapa kwenye Kitabu hiki cha Ufunuo ndicho Kitabu pekee (Hebu nirudie hilo.) ambacho Mungu alikiidhinisha. Basi jambo la kwanza alilofanya ni kufunua Uungu Wake, Naye anaufunua kikamilifu. Na kusema, “Yeyote atakayeondoa lolote kutoka kwenye Hiki au kuongeza lolote Kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kutoka katika Kitabu cha Uzima. Heri yeye asomaye, ama yeye asikiaye. Na amelaaniwa yeye atakayeongeza jambo moja Kwake au kuondoa lolote kutoka Kwake.” Haya basi, kwa hiyo mnaona sehemu yenye hatari. Kwa hiyo kamwe usiongeze lolote kwenye Hicho; kiache tu jinsi kilivyo, na uzidi kusonga mbele.

⁹³ Roho atakufunulia ikiwa utakuwa tu mnyenyekevu, mwombe. Mnaona? Hiyo ni kweli. Sasa, kwa hiyo si kigumu. Mungu . . . Yesu alimshukuru Baba kwa . . . akisema, “Nakushukuru Wewe, Baba, kwamba umeyaficha mambo haya kutoka kwa macho ya marabi, na maaskofu, na makadinali, wasimamizi wakuu, na—na umewafunulia watoto wachanga watakaojifunza.” Mnaona?

⁹⁴ Hivyo ndivyo unavyotaka. Ni ufunuo wa Mungu unaoweza tu kuja kama Yeye alivyosema pale, “Watu husema kwamba Mimi ni nani?”

Akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye Hai.”

⁹⁵ Akasema, “Simoni, kamwe hukujifunza hayo katika seminari. Unaona? Hakuna mtu aliyewahi kukwambia hilo. Hilo limekuja, lilikuwa ni ufunuo kutoka Mbinguni. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

⁹⁶ Huo hasa ndio ufunuo ambao Habili alikuwa nao hapo mwanzo. Ni ufunuo; ulikuwa wakati huo, ungali ni ufunuo, na daima utakuwa ni ufunuo. Hiyo ni kweli.

⁹⁷ Sasa, tunaona hapa ya kwamba yeye alikuwa mwanamke sasa, na *mwanamke* anawakilisha “kanisa.” (Hiyo ni kweli? Kristo anakuja kwa ajili gani? Bibi-arusi, mwanamke, bikira safi.) Naye maskini mwanamke huyu hapa, alidai kwamba yeye ni Kanisa la Mungu; bali, kile alichokuwa, alikuwa amepambwa utajiri na lulu, na kila kitu, naye alikuwa na kikombe cha

uchafu wa uasherati wake, ambapo aliwafanya wafalme wote wa duniani kulewa na mvinyo wake. Hiyo ni kweli?

⁹⁸ Sasa, tunamwona hapa kwamba anaitwa “Yezebeli.” Naye Yezebeli, maovu ambayo Yezebeli alifanya, mara alipopata madaraka miongoni mwa Israeli, aliwaua na kufanya kila alichoweza, na—na kujenga madhabahu yake mwenyewe. Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo kanisa Katoliki lilivyofanya hasa. Ndivyo hasa. Lakini sasa hebu tusome mbele kidogo tu. Hili litawadumaza. Wakati mwingine ukidumaa, utakula zaidi kidogo.

. . . yeye ajiitaye nabii mke, (Sasa, kama akisema, “Mimi ndimi mfasiri pekee wa Neno.”) na kuwafundisha na kushawishi watumishi wangu kufanya uasherati, . . . kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.

⁹⁹ Yule ndugu aliyeuliza juu ya “yule nyoka,” kuhusu “kula tunda katika bustani la Edeni.” Unaona ni kitu gani (Sivyo?) aliposema, “kula,” hapa. Jambo ni kwamba, ilikuwa ni kiroho, unaona. Na ninii . . . na . . .

Nami nimempa muda ili atubu uzinzi wake—uzinzi; wala hakutubu.

Tazama. Nitamtupa juu ya kitanda, . . . (Ni kitanda cha aina gani? Cha kilimwengu. Hivyo ndivyo hasa alivyo siku hizi). . . na hao wazinio pamoja naye, wapate dhiki kubwa wasipotubia matendo yao. (Hiyo ni kuingia katika Dhiki Kuu.)

Nami . . . nitawaua watoto wake kwa mauti; . . .

¹⁰⁰ Whaa! Ati akina nani wake? Maskini msichana huyu alikuwa na watoto. Sasa Ufunuo 17. Ni wangapi wenu . . . ? Ninyi nyote mlikuwa hapa jana usiku, nadhani. Vema. Ufunuo 17, maskini kahaba huyu, kanisa Katoliki, aliitwa “kahaba,” naye alikuwa “mama wa makahaba.” Wasingekuwa wavulana, walikuwa ni *makanisa*.

¹⁰¹ Sasa ni wapi kanisa la Kilutheri, haya yote yalitoka wapi? Kila dhehebu lilitoka wapi? Chanzo chake ni wapi, Laodikia? Unikolai hatimaye uliingiana nalo; hicho ni kitu kile kile tena. Huwezi kukizuia, ndugu. Loo, Eliya alikikemea kitu hicho katika siku zake. Yohana akakikemea katika siku zake. Naam, bwana! Msiwaze mioyoni mwenu kwamba, “Tunaye baba, ndiye Ibrahimu: kwa maana nawaambia Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Mnaona? Kamwe halizuiliki.

¹⁰² Sasa, alikuwa na watoto. Hivi Yezebeli mwenyewe alikuwa na watoto? Naam, bwana! Sikilizeni:

. . . nitawaua watoto wake . . .

¹⁰³ Kitu gani? Kanisa Katoliki, watoto wake ni dhehebu la Kiprotestanti. Mnaona, kweli kabisa, maana wanafanya jambo

lile lile. Wanabatizwa moja kwa moja kwake kwa ubatizo bandia, ubatizo usio wa kimaandiko; kupeana mikono badala ya Roho Mtakatifu; “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” badala ya “Yesu Kristo.” Na kufanya tu kila kitu kinyume na Biblia. Bado! Nao wanaingia moja kwa moja ndani yake.

¹⁰⁴ Binti yake aliitwa Athalia, A-t-h-a-l-i-a. Alikuwa na ninii yake. . . Yeye, Yezebeli, alimfanya Athalia kuolewa na Yehoram, mwana wa mfalme wa Yuda, na karibuni madhabahu ya Mabaali yalikuwa yamesimama katika Yerusalemu. Sasa, haiwabidi kuiendea historia kwa hayo, hiyo ni Biblia. Mnaona? Binti yake, Athalia, aliolewa na mwana wa Yehoshafati, ambaye alikuwa ni Yehoram. Nao binti zake wakafanya jambo lile lile alilofanya.

¹⁰⁵ Loo, jamani! Hivi hamwezi kuona? Kuona jinsi hayo madhehebu yalivyofanya, ndugu? Yalirudi moja kwa moja kupitia Luther na hao wengine, hasa kabisa, na kujiundia madhehebu badala ya kumruhusu Roho Mtakatifu. Nayo Pentekoste ilifanya jambo lile lile hasa. Wasingemwacha Roho Mtakatifu aendelee na afanye atakavyo, na kuendelea; na kila nuru inayokuja, waichunguze tu kwa Neno, na kuendelea. Wasingemwacha Roho Mtakatifu aongoze, iliwabidi kuunda dhehebu na kukatiliwa mbali na kitu kingine chochote ambacho kingekuja. Wakarudi moja kwa moja nyuma na kuolewa na kitu hicho tena! Vivyo hivyo hasa. Tutakapoufikia wakati huo, angalieni tu ni kitu gani kinachowangojea huku chini barabarani hapa. Mnaona? Akaolewa moja kwa moja tena! Yesu alisema hapa, “Nanii wake. . . Yezebeli huyu, yeye anajiita ‘nabii mke,’ nami nitamtupa katika kitanda cha kilimwengu, na kuwaua watoto wake pia” (Sasa, ni ya aina gani. . .?) “kwa mauti.”

¹⁰⁶ Ni nini. . . watoto wake watauawa kwa mauti ya namna gani? Mnaona hao wamekufa sasa! Wamekufa kiroho! Hawana ufunuo! Wanalijua dhehebu lao, wanajua katekismo yao, wanajua fundisho lao la kanisa; bali inapofikia kumjua Mungu, baadhi yao hawajui kumhusu kuliko Mhotentoti angejua kuhusu hekaya za Kimisri; hiyo ni kweli, inapofikia kumjua Roho Mtakatifu hasa. Wakishangaa; wanamwita. . . wakitaka kumwita Roho wa Mungu “mpiga ramli,” ama “ibilisi,” wa. . . kwa kuzitambua roho, na mambo kama hayo, na kutoa pepo. “Mbona, yeye si wa dhehebu letu. Kundi hilo, loo, brrruu.” Mnaona, kamwe hawajui. Halafu wanalibandika ji—jina la “Yesu Pekee,” ama namna fulani ya “mtakatifu anayejibingirisha,” ama—ama namna fulani ya kitu kama hicho. Kamwe hawajui!

¹⁰⁷ Nayo saa imekaribia sana wakati kitu hicho kitakapowekwa wazi. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu atakianika kwa hakika tu kama ninavyosimama nyuma ya mimbara hii, maana atawanyakua watoto Wake kwa hakika kama ninavyosimama papa hapa. Mungu Mbinguni anajua hilo. Mkiniamini mimi

kuwa ni nabii wa Bwana, mtumishi wa Bwana, nisikilizeni mimi. Imekaribia sana. Naam, bwana.

108 “Watoto wake watauawa kwa mauti ya kiroho.” Waangalieni: baridi na wa kawaida. Angalieni ninii. . . angalieni ninii yetu. . . Haitubidi kuzungumza juu ya Wabaptisti na Wapresbiteri, tunajua wamekuwa wafu kwa miaka kadhaa. Kile. . .

109 Wakati Luther alipokuwa na uamsho wake, kuhesabiwa haki, kama angalininii. . . Kama angaliendelea, huu—huu uamsho mkuu wa Kipentekoste sasa ungekuwa ni wa kanisa la Kilutheri. Hiyo Nuru ingalikuja kwa utakaso, kama Wesley angalifuatilia. Yeye. . . Luther asingeweza kuifuata hiyo. La, bwana, hao tayari ni Walutheri.

110 Kwa hiyo basi Wesley akaja. Baada ya Wesley kufariki, basi ilikuwaje? Waliunda dhehebu juu ya huo, na kuunda Methodisti ya Kiwesley, Wes-. . . ya Kishamba, loo, kila namna ya Wamethodisti. Mnaona? Na wakati. . . Alikuwa na uamsho mkuu sana, bali wakati walipolitupa dhehebu ndani ilikuwaje wakati Pentekoste ilipokuja ikinena kwa lugha na kuleta kule kurudishwa kwa karama? Wasingeweza kusogea; waliwaita ibilisi.

111 Sasa Wapentekoste wamefanya nini? Jambo lile lile walilofanya! Nao wako wapi? Wamekufa tu kama msumari wa mlango. Naam, bwana! Hiyo ni kweli kabisa. “Nitawatupa watoto wake juu ya kitanda cha—juu ya kitanda cha mauti, na kuwaua.” Vema, hebu—hebu niwasomee hilo mpate kuona hapa, ninaamini ilikuwa ni kifungu cha 22:

Nami *nitamtupa juu ya kitanda, na hao wazinio pamoja naye wapate dhiki kubwa, (ile—ile Dhiki Kuu).* . .

112 Hilo ndilo linaloendelea. Sasa kumbukeni, hebu nisimame hapa kwa dakika moja, ile Dhiki Kuu ni wale—wale watakaotupwa mle ndani, ni wale watu ambao ni wanawali waliolala ambao hawakuwa na mafuta kwenye taa zao; hata hivyo walikuwa wafuasi wa dhehebu fulani, watu wazuri, walienda kanisani, kila kitu; bali wakaja kununua mafuta, ila ilikuwa imechelewa sana basi. Mnaona, kumtupa kwenye Dhiki Kuu, ataingia humo, kanisa Katoliki litaingia mle, watoto wake wote wataingia pamoja naye, katika ile Dhiki Kuu.

. . . *wasipotubia matendo yao.*

113 Sio—sio watoto walio mle ndani; bali kanisa lenyewe, hao ni watoto wake (ni madhehebu), sio watu walio mle, kama maskini Wakatoliki, Wabaptisti, Wapresbiteri, ama Wapentekoste. Ninawahurumia. Ninii tu, “Vema, mimi. . .”

“Wewe ni Mkristo?”

“Vema, mimi ni Mpresbiteri.” Loo!

114 Hilo halina uhusiano wowote nalo kuliko kusema “nguruwe mwenye matandiko alikuwa ni farasi wa mashindano.” Kwa hiyo ungefanya nini kuhusu hilo kamwe? Mbona, hakuna kitu hata kidogo. Sikumaanisha kufanya mzaha hivyo, hiyo ni . . . hapa si . . . sio mahali pa mizaha, hii ni—hii ni Injili. Mnaona? Nilitaka tu kutoa mfano. Mnaona, lakini hiyo—hiyo ni kweli. Mnaona, hawana—hawana uhusiano wowote nalo kamwe.

“Mimi ni Mpentekoste.”

115 Hilo halina uhusiano wowote nalo kabisa. Ungeweza kuwa mfuasi wa madhehebu yao mia nne na kumi na moja, lakini je, wewe ni mwana wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili? Kweli, unampenda kila mtu kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako, na unampenda Mungu, nawe kila siku. . . haijalishi mtu yeyote anakufanyia nini? Kama ukishikwa na hamaki na kusema, “Huum!” kama msumeni uvumao, inaonyesha tu Roho Mtakatifu ameondoka, kama uliwahi kuwa Naye.

116 Angalieni:

. . . asije *akatubia matendo* hayo.

Nami nitawaua watoto wake kwa mauti; . . .

117 “Watoto wake,” wa Yezebeli. Sasa, Yezebeli alifanya nini? Alimwoza binti yake kwenye tabaka lingine (la Yuda) huko, huko Yuda. Sasa angalieni matumizi ya kiroho. Labda ninaweza kuichora. Hapa, angalieni hili kwa makini sana sasa:

118 Huyu *hapa* Yezebeli, na Israeli. Lakini hii *hapa* ni Yuda, aina tofauti hapa, kwenye nyingine; huyu ni wa Yehoshafati hapa. Vema. Sasa, huyu *hapa* alikuwa ni Ahabu; sasa huyu hapa Yezebeli papa *hapa* ndani. Sasa, anaingia *hapa* ndani na kuwafanya Israeli wote kuingia katika uzinzi.

119 Hivyo ndivyo kanisa Katoliki lilivyofanya hasa huko nyuma katika siku zake wakati Konstantino alipowaunganisha Wanikolai (wale baridi wa kale *hapa* juu) katika—kwenye—kanisa na upagani, na kuunda namna ya Ukristo wa kipagani. Sitaki kuudhi hisia zenu, enyi Wakatoliki, bali ninawajibika mbele za Mungu. Hivyo ndivyo tu lilivyo kanisa Katoliki, ni Ukristo wa namna ya kipagani: ushirikina, na sanamu, na kadhalika. Hiyo ni kweli kabisa, ni utaratibu wa kipagani tu. Sasa, hiyo ni kweli. Kama ninakufa dakika hii, hiyo ni kweli. Na Waprotestanti moja kwa moja katika kitu kile kile, katika tabaka jingine tu.

120 Sasa angalieni kile Yezebeli alichofanya. Ndipo, mnaona, i—ibilisi. . . Alikuwa amejitolea sana, akawachukua binti zake. Alikuwa na binti aliyezaliwa *hapa*, naye binti huyu anaenda *hapa* kwa mtu huyu mashuhuri mtakatifu na kumchukua na kuolewa na mwanawe; naye analeta kitu kile kile *hapa* kutoka kwa Yehoshafati, kwenye sehemu hii.

¹²¹ Sasa, Wanikolai halisi, Wanikolai, maskini wale baridi waliotaka dhehebu hilo, waliolewa katika hilo *hapa*. Na sasa angalieni jambo lile lile. Walimchukua Yezebeli *hapa* (kanisa Katoliki), na *hapa* chini anamchukua binti yake (madhehebu yake) na kufunga ndoa nao kule chini, na kuwafanyia jambo lile lile. “Kuwaau watoto wake kwa mauti,” mauti ya kiroho. Wanajiundia dhehebu hata kufa, na muda si muda mwajua, Roho yote imeondoka.

¹²² Niambieni. Hebu niwaulizeni tu jambo moja, mwanahistoria yeyote hapa, ambao najua kuna watano ama sita wenu mlioketi hapa. Ninawatakeni mje na kutoa Andiko moja ama—ama fungu moja la—la historia, ambapo lolote la makanisa yaliyopata kuanguka na kuingia kwenye dhehebu lilipata kuinuka tena kwa uamsho. Niambieni. Wakati walipojiundia dhehebu, je, waliwahi kuwa na uamsho baada ya kuunda dhehebu? La, bwana! Roho aliwaacha. Ninajumuisha Pentekoste.

¹²³ Wakati Baraka za Kipentekoste ziliposhuka, nanyi nyote mkanena kwa lugha, ninyi watu wa zamani, mkiwa na hizo Baraka kuu za Kipentekoste na kadhalika, zilizoshuka. Baada ya kitambo kidogo mlikuwa na kile mlicheoita Baraza Kuu. Utaratibu ni sawa, bali si dhehebu. Muda si muda mwajua, msingeweza kulivumilia, iliwabidi kurudi moja kwa moja mkawa “mtoto wa . . . Shetani,” na kujiundia dhehebu.

¹²⁴ Ndipo Nuru nyingine ikatokea, kuhusu Jina la Yesu Kristo. Ndipo wote wakakwama, na kusema, “Mungu abarikiwe, kama huna jina la Yesu, unaelekea kuzimuni. Nasi tunalo, wala ninyi hamna.” Walifanya nini? Walikufa tu papo hapo njiani mwao; wakaunda dhehebu kutokana nalo. Mnaona? Badala ya kuiachilia Nuru ienee kanisani mwote, ingechukua mahali pake moja kwa moja. Lakini mlijiundia dhehebu. Ni kitu gani? Mtoto wa Yezebeli. Nao wote wakafa, pamoja.

¹²⁵ Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Hivi Assemblies of God, ama Umoja, ama—ama lolote la hayo mengine limewahi kuinuka katika uamsho mkubwa wa umoja? Hata kidogo! Huu uamsho wa mwisho ndio kwanza upite, ambapo Roho Mtakatifu alishuka pale mtoni (wengi wenu wanaoketi hapa sasa hivi) katika mwaka wa 1933, na ibada hii kuu ya uponyaji ilikuwa itukie, kasema, “Ungeenea kote ulimwenguni,” nao kamwe haukupitia kwenye dhehebu lingine lolote hata kidogo. Mungu alienda nje ya milki na kumwinua aliyekuwa kafiri, karibu hivyo, kuanzisha uamsho huo. Basi angalieni kile umefanya! Mnaona?

¹²⁶ Hayo madhehebu, mara yanapoundwa, yamekufa. Yeye alisema, “Nitawau watoto wake kwa mauti.” Loo, jamani! Ninawajua . . . Naomba msinionee vibaya, lakini mimi . . . Kama nikijua Hili wala nisiwaambie, mimi ni mnafiki duni sana, na Mungu ataniwajibisha Kwake. Ninataka kuwa kama Paulo,

“Kutojiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.”
Hiyo ni kweli. Vema. Vema.

127 Sasa, nao wakajenga madhabahu Yerusalemu. Sasa ninataka kuona . . . Ndipo hapo Yezebeli alipoolewa na Ahabu, aliwaletea Israeli sanamu wapate kuzisujudia. Vivyo hivyo na fundisho la Wanikolai, kuoia katika upagani; wakashusha Jupita, wakampandisha Petro; na Venasi, hata Mariamu; na kama vile Biblia ilivyosema, “Aliwafanya Israeli wote kutenda dhambi.”

128 Vivyo hivyo kanisa Katoliki limewafanya binti wote kuolewa na dhehebu, na jambo hilo lote ni dhambi, kama vile Yezebeli kwa binti yake. Vema. Na katika kufanya hivi wakati ukasisi ulipowekwa, naye Papa Boniface—Boniface III akachukua kiti chake, basi walikuwa na mu—mungu kwenye kiti cha enzi, hawakuwa na haja tena ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kanisani. Hiyo ni kweli. Walikuwa na kanuni zao za imani na utaratibu, na kuendelea.

129 Basi wakati dhehebu lilipokubali fundisho lile lile la sharti, waliuondoa uhuru wa Roho Mtakatifu kanisani, Baptisti, Presbiteri, Methodisti, na kadhalika. Hakika walifanya hivyo! Na hatimaye tunawaona wakinyauka na kufa kama vile Yesu alivyosema juu ya mzabibu. Sasa, Roho Mtakatifu wote katika ishara na maajabu aliwekwa nyuma katika siku zilizopita. Nao wamekuwa tajiri, kama huyo mwanamke alivyofanya. Kwa hiyo akaufanya ulimwengu mzima wote kutenda dhambi, kwa sababu ameenda kwa kila taifa, yeye na binti zake. Hiyo ni kweli.

130 Sasa mwangalie akimwita katika wakati mwingine wa kanisa sasa. Mwangalie akimwita. Mwangalie akimsihi hapa chini mwishoni, kuwatoa Masalio Wake, “kwa ajili ya Wateule,” wachache tu, kwamba hakuna mtu angeokolewa kama . . . wengine sivyo.

131 Kama ilivyoandikwa katika Ufunuo 13:6. Mngetaka kufungua hapo kwa dakika moja? Kwamba Yeye alisema Yeye . . . kwamba “Mwanamke huyu aliwafanya wote kupokea alama (mnyama huyu aliwafanya), akawafanya wote kupokea alama (wote maskini, wakuu, wowote wale), alama ya mnyama,” ambayo ilikuwa ni Kanisa Katoliki la Kirumi.

132 Ama hiyo au walifanya sanamu . . . Ufunuo 13:14, walifanya sanamu ya mnyama. Nyinyi—nyinyi . . . Nadhani nyote mnasoma hilo. Kama hamjasoma, mbona, tutafungua moja kwa moja na kulisoma. Ufunuo 13:14:

Naye akawadanganya wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kufanya mbele ya huyo mnyama; (Huo ni muungano huu wa kanisa.) . . . na kufanya mbele ya huyo mnyama; akawaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la mauti (upagani) . . . na lilikuwa la upanga,

naye akaishi . . . (kupitia kwa upapa, Rumi ya kipagani kuwa Rumi ya kipapa. Mnaona?)

133 “Kumfanyia sanamu.” Ingekuwa ni nini? Ni kile tu wanachofanya sasa hivi, kweli kabisa, wakiingia katika muungano huu wa makanisa, “Makanisa yote yako kwenye shirika hili, yote yanaingia kwenye kundi moja.” Sasa wanaitafuta Biblia. Naye Papa Yohana amewaalika wote warudi. Askofu mkuu wa Canterbury, wote wanaenda huku na huku. Jambo la kwanza mwajua, kitu hicho chote kinarudi moja kwa moja kwa *Mama*, kwa kuwa hao tangu mwanzo ni makahaba. Mnaona? Wanasema, “Sote tutajiunga pamoja katika mwamsho mmoja kupigana na Ukomunisti.” Wala hawajui ya kwamba Mungu aliinua Ukomunisti (ninaweza kuthibitisha hilo kwa Biblia hii.) na hata akaweka niani mwao wapate kulipizia watakatifu kisasi, cha damu waliyokuwa wamemwaga juu ya nchi. Mungu aliinua Ukomunisti kama vile alivyofanya Mfalme Nebkadreza ku—kuwarudi Israeli. Aliinua Ukomunisti, na siku moja utalipua Rumi moja kwa moja uiondoe kwenye ramani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni kweli kabisa. Mungu alisema hivyo. Hiyo ni kweli.

Mimi ninaupinga ukomunisti; ni upinga Mungu. Hakika ndivyo ulivyo. Lakini msilishughulikie sana hilo Pazia la Chuma, bali liangalieni hilo pazia la zambarau. Someni *Kitabu cha Wafia Imani* cha Foxe nanyi mtaona hili, hiyo ni kweli.

134 Sasa hebu tuone ni wapi sisi . . . Halafu basi mnaona hapa sasa ya kwamba aliwafanya wote (matajiri, maskini) kupokea alama; bali kuna tabaka moja ambalo hakuweza kugusa. Mnajua hilo? Ufunuo 13: . . . 8.

135 Sikilizeni hili. Hebu nisome hili:

Kisha nikasimama juu ya mchanga wa bahari, nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, . . . juu ya pembe . . . vilemba, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. (Hivyo ni vile vilima saba; tuliyachukua yote jana usiku, mwajua.)

Na yule mnyama uliyemwona alikuwa mfano wa chui, . . . miguu yake ilikuwa kama—kama miguu ya dubu, na kinywa chake . . . kama kinywa cha simba: yule joka (Aliyekuwa yule ibilisi mwekundu aliyesimama mbele ya mwanamke apate kumla pamoja na mtoto wake, ambaye alikuwa ni Rumi, sote tunajua hilo.) . . . *akampa . . . nguvu na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi.*

Nikaona kimoja cha vichwa vyake kama kwamba kimetiwa jeraha la mauti; (upagani, mnaona) . . . na jeraha lake la mauti likapona: (upapa unapachukua mahali pake, ukiunganishwa na Ukristo, pamoja na Wanikolai) . . . dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.

136 Ukamoliki umeenea kwenye kila taifa chini ya mbingu. Hiyo ni kweli. Kama Danieli alivyosema kuhusu chuma ikiingia kwenye udongo, na kadhalika.

137 Nami nitawapa jambo dogo juu ya hiyo, hiyo “chuma na udongo.” Hivi mliona, ama je, nimewahi kuwanukulia, katika lile kongamano kuu la mwisho walilokuwa nalo hapa juu ambapo Khrushchev alivua kiatu chake na kupiga meza nacho? Kulikuwako na mataifa matano ya kimashariki waliokusanyika kule, kulikuwako na mataifa matano ya kimagharibi. Khrushchev aliyaongoza mataifa ya mashariki, Eisenhower akayaongoza mataifa ya magharibi; hao hapo wale viongozi wawili wakuu, vile vidole viwili vikubwa. *Khrushchev*, katika Urusi, linamaanisha “udongo.” *Eisenhower*, katika Mare- . . . katika Kiingereza, linamaanisha “chuma.” Tuko kwenye mwisho.

Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake: nao. . . (Huo ndio ujumbe wetu unaofuata hapa maskanini, mnaelewa.) . . . nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyo? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?

138 Kwa maneno mengine, angalieni hapa. Eisenhower ana— ana jina kubwa hapa katika Marekani hii, bali huko Rumi yeye si kitu; Urusi, yeye si kitu. Khrushchev ni mkubwa Urusi, bali Marekani yeye si kitu. Lakini kuna mtu mmoja ambaye ni mkubwa kila mahali, huyo ni papa (Hiyo ni kweli.) “Hebu tuungane pamoja, na tuje pamoja.”

Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu. . . makufuru; . . . akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili.

Akafunua kinywa chake na kumtukana Mungu, (na “kufundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu; wakaidi, wapenda anasa; wenye mfano wa utauwa, wakikana Nguvu zake”) . . . na wakalitukana jina lake, (Wakachukua “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” badala ya “Bwana Yesu Kristo.” Mnaona.) . . . na maskani yake, nao waliokaa huko. . . mbi— mbinguni.

Tena akapewa kufanya vita dhidi ya watakatifu, (hayo hapo yale mateso yanaibuka) . . . na kwashinda: akapewa uwezo juu ya kila jamaa . . . lugha na, mataifa.

Na watu wote wakaao juu ya nchi—nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. (Loo, loo, loo, loo, loo, loo.)

139 “Kuwekwa misingi ya dunia.” Majina yetu, kama yaliwahi kuwa kwenye kile Kitabu, yaliwekwa huko nyuma. Yesu alisema,

“Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu,” (Hiki ni Chakula, mnaona.) “na mgeni. . .”

¹⁴⁰ Ndipo anaweza kusema, “Vema, ndio kwanza tu nijiunge na kanisa, mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe.” Hicho si Chakula cha kondoo.

¹⁴¹ *Hiki* hapa Chakula cha kondoo, “Kuketi pamoja katika mahali pa Kimbinguni katika Kristo.” Loo, Yeye ni wa ajabu sana! Sivyoy? Vema.

¹⁴² Sasa hebu tumalizie upesi sana kwa kuwa ni, naam, wakati umepita sasa. Vema. “Lakini nasema. . .” Hebu tuone sasa, ninacho kifungu cha 23:

Nami nitawaua watoto wake kwa mauti, na makanisa yote watajua ya kuwa mimi ndiye achunguzaye viuno na mioyo: Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake.

Lakini nawaambia ninyi wengine mlioko Thiatira, wowote wasio na mafundisho haya, . . . (Yalikuwa ni mafundisho ya namna gani? Madhehebu, maaskofu, na maaskofu wakuu, na mapapa, mnaona.)

¹⁴³ “Wasio na mafundisho haya.” Sasa, Biblia, tuliona jana usiku ya kwamba Israeli, wakipitia Moabu, hawakuwa ni taifa. Waliishi juu ya uso wa nchi, nao walikuwa watu, huru. Hiyo ni kweli? Mfano; wazururaji, katika mahema na kadhalika. Makundi ya Kipentekoste ni vile vile, pentekoste ya kweli, wakitanga-tanga mahali mahali. Mnaona? Vema.

. . . wasio na mafundisho haya, (lakini wamejiundia madhehebu, na kufanya shirika kubwa kutoka kwake) . . . wasio na haya. . . wasiozijua fumbo za shetani, . . .

¹⁴⁴ Sasa kumbukeni tulipata mahali kiti cha Shetani kilipokuwa. Jana usiku tulimchukua moja kwa moja hata mwanzo. Kiti chake kilikuwa wapi mwanzoni? Babeli. Nayo Babeli. . . Wakati u—ukasisi, mfalme-kuhani wa Babeli, alipokuwa akifukuzwa na Wakaldayo washindi, alihamia Pergamo na kuweka kiti chake. Mnaona, akahamisha kiti chake kutoka nchi ya Shinari hadi Pergamo. Tulisoma hilo moja kwa moja katika historia jana usiku. Ndipo sasa hapo akaanza, akaliunda kanisa Katoliki, ambalo lingali ni mama Babeli. Vema, “Kiti cha Shetani.”

. . . na kiti cha Shetani, kama vile wasemavyo; sitaweke juu yenu mzingo mwingine.

¹⁴⁵ “Hakutakuwako na mzingo mwingine; ni ule tu mlio nao tayari.” Maskini hawa wachache walio mle ndani, mnaona,

ambao wamebanwa kabisa katika Wakati huu wa Giza. Sasa ni karibu sana miaka elfu moja mia tano waliyopitia hayo.

Ila mlichio nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja.
(Kwa maneno mengine, “Mngali mnayo Baraka ya Kipentekoste mioyoni mwenu. Ishikilieni hiyo hata nitakapokuja kuwapa faraja, kwa kuwa wakati huu mwingine ndio kwanza unakuja katika wakati ufuatao.”)

. . . yeye ashindaye, na kuyatunza maneno yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa:

Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma; kama chombo cha mfinyanzi watawavunja vipande-vipande: kama mimi nami nilivyopokea mamlaka kutoka kwa Baba yangu.

146 Unaona, Kanisa hilo, itakuwaje wakati hilo Kanisa la Nyakati za Giza litakaposimama katika hukumu dhidi ya kundi hilo la kipagani la . . . huko nyuma? Watapondwa-pondwa kwelikweli! Hiyo miguu ya shaba itawakanyaga-kanyaga kule, nawaambia! “Atawavunja vipande-vipande,” Biblia ilisema.

Nami nitampa ile nyota ya asubuhi. (Mnajua hiyo ni nini, siyo? *Kristo* ndiye “Nyota ya Asubuhi.” Vema.)

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.

147 Loo, jamani! Hivi hamna furaha! Tumechelewa kidogo tu. Nina mengine zaidi, nitayachukua labda kesho usiku, juu ya hii miaka elfu mbili pale.

Lakini Yeye ni Yungiyungi la Bondeni,
Nyota ya Asubuhi yenye Kung’aa,
Yeye ndiye mwema zaidi ya elfu kumi nafsini mwangu;
Yunguyungu la Bondeni, naona ndani Yake pekee,
Yote ninayohitaji . . . kunifanya mzima kabisa.
Katika huzuni Yeye ndiye faraja yangu, katika shida Ndiye msaada wangu,
Huniambia nimsukumie kila shida. Haleluya!
Yeye ni Yungiyungi la Bondeni, Nyota ya Asubuhi yenye Kung’aa,
Yeye ndiye mwema zaidi ya elfu kumi nafsini mwangu.

148 Je, mnampenda? Loo, ni kwamba tu:

Nampenda, na- . . . (Sasa hebu tumwabudu sasa, maneno hayo yote yanayokata-kata na huu Ujumbe.)
Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁴⁹ Hivi Yeye si ni wa ajabu! Nampenda. Sasa, mambo niliyoshindwa kuyafikia, yatakuwa kwenye vitabu, hakika, maana hatuwezi kulileta kanisa lote katika usiku mmoja. Kidogo niliinyamazisha kidogo usiku wa leo, kwa sababu ya kupwelewa kidogo na sauti. Lakini, loo, hivi Yeye si ni wa ajabu! Loo! Hmm!

Wapo watu karibu kila mahali,
Ambao mioyo yao imewaka moto,
Kwa moto ulioshuka Pentekoste,
Uliowasafisha na kuwafanya safi;
Loo, unawaka moyoni mwangu sasa,
Loo, utukufu kwa Jina Lake!
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Loo, mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao, Haleluya!
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

¹⁵⁰ Hivi una furaha? Ninakumbuka nikitoka Chattanooga siku moja usiku; nayo ndege ililazimika kutua huko—huko—huko Tennessee, huko Memphis. Waliniweka kwenye ile hoteli kubwa, nzuri kule. Nao wakanipigia simu, kasema, “Ndege itaondoka saa—saa moja, kesho yake asubuhi.”

¹⁵¹ Nami nilikuwa nikipeleka barua posta; nikija nyumbani, nikiwaandikia baadhi ya rafiki zangu. Basi wakati nikishuka, Roho Mtakatifu akasema, “Endelea kutembea.” Nikaendelea tu, nikafika kwenye mtaa wa watu weusi.

¹⁵² Nilikuwa nimesimama kule chini, nikawazia, “Jamani! Angalia hapa, wakati umewadia wa ndege hiyo kuondoka.”

¹⁵³ Naye Roho Mtakatifu akaendelea kusema, “Endelea kutembea.” Kama tu vile alivyofanya huko chini mwituni hivi majuzi, mwajua. “Endelea tu kutembea.” Kwa hiyo nikaendelea kutembea.

¹⁵⁴ Iitokea niliangalia huko chini kabisa, katika moja ya vile vibanda vya watu weusi ambamo watu weusi walikuwa wakiishi, maskini, huko chini. Naye *Shangazi Jemima*, mfano wake hasa, amefunga shati la kivulana kichwani mwake, amegemea ninii . . . namna hiyo.

¹⁵⁵ Nami nilikuwa nikienda pale nikiimba:

Mimi . . . wao, mimi ni mmoja wao,
 nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao, Loo, Haleluya! (“Nawe
 wataka nini, Bwana?”)

Mmoja wao, mimi ni mmoja wao, (Hivi
 mnaamini katika kuongozwa na Roho?
 Naam, hakika.)

Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

156 Ni karibu miaka kumi na minne iliyopita sasa. Alikuwa akiangalia juu ya ua. Nilikuwa karibu, loo, nusu jengo la mji kutoka kwake, nami nikamwona bibi huyo mzee mweusi akiniangalia papo hapo chini, mwajua. Vema, niliendelea tu, nikaacha kuimba, nikaanza kushuka chini. Nikamkaribia, machozi makubwa mno kwenye hayo mashavu makubwa manene; akianiangalia, kasema, “Habari za asubuhi, Kasisi!”

157 Nikageuka, nikasema, “U hali gani, Shangazi?” Naye akasema . . . Nikageuka, alikuwa akicheka, alikuwa na tabasamu kubwa usoni mwake. Nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?” Huko chini Kusini, mwajua, *mhubiri* ni “kasisi.” Kasema . . . Nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?”

Akasema, “Nilijua ulikuwa unakuja!”

Nami nikasema, “Ulijuaje hilo? Kwani wanijua mimi?”

Akasema, “La, bwana.” Naye akasema, “Ninajua ulikuwa unakuja.” Kasema, “Ulipata kusikia ile hadithi ya mwanamke Mshunami?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

158 Naye akasema, “Vema,” kasema, “Mie ni mwanamke wa aina hiyo.” Akasema, “Basi Bwana alinipa mtoto mchanga, nami nikamwambia . . . nikamwambia ya kwamba nitamlea.” Kasema, “Mimi ni mwanamke maskini. Ninafua nguo na kuwafanyia kazi wazungu nipate riziki.” Akasema, “Na Yeye aliniambia ya kwamba a—atanipa mtoto mchanga, nami nikamwambia nitamlea.” Kasema, “Nilimlea vizuri nijuavyo, lakini” kasema, “Kasisi, yeye alishikana na kundi baya. Akashikwa na ugonjwa, wala hatukujua kitu kuuhusu.” Kasema, “Akaugua vibaya. Naye yuafa, mle ndani kitandani.” Kasema, “Ampoteza fahamu sasa, siku mbili.” Kasema, “Daktari alikuja akasema, ‘Tayari umeula moyo wake na kadhalika, ukaingia kwenye mkondo wake wa damu, ni mbaya sana hata umemwangamiza; hivi kwamba vitu wanavyompa visingemsaidia sasa.’” Kisha kasema, “Yuafa.” Halafu kasema, “Kamwe siwezi kuvumilia kumwona akifa, mwenye dhambi.” Halafu kasema, “Niliomba na kuomba,” kasema, “usiku kucha niliomba.” Kasema, “Ampoteza fahamu, hajui chochote.” Kasema, “Hakujitambua kwa siku mbili.”

159 Kasema, “Niliomba, nikasema, ‘Bwana, ulinipa mtoto huyu’ kisha kasema ‘kama ulivyomfanyia yule mwanamke Mshunami.’”

Kasema, ‘Yu wapi Eliya Wako? Yu wapi . . .?’ Kasema, ‘Vema, ki—ki wapi kitu cha kunisaidia?’”

¹⁶⁰ Kisha akasema, “Nilishikwa na usingizi nikiwa magotini mwangu.” Kisha kasema, “Bwana akasema nami, katika ndoto yangu,” naye akasema, “Nenda kasimame karibu na lile lango. Basi kutakuwako na mtu akishuka kuja mtaani, amevaa kofia ya hudhurungi na suti nyeusi.’ Akasema, ‘Yeye atazungumza nawe.’”

¹⁶¹ Ndipo akasema, “Nimekuwa nikisimama hapa tangu kabla ya mapambazuko.” Nao mgongo wake ulikuwa umelowa umande. Naye akasema, “Ndipo nikakuona ukija umevaa kofia hiyo ya hudhurungi,” akasema, “ila ulipaswa kuwa umebeba mkoba mdogo.”

¹⁶² Nikasema, “Niliuacha hotelini.” Mnaona? Nami nikasema, “Ati mvulana wako ni mgonjwa?”

Kasema, “Yuafa.”

Nikasema, “Jina langu ni Branham.” Nikasema, “Hivi unanijua?”

Akasema, “La, bwana, Kasisi Branham, si—sijawahi kukusikia.”

Nikasema, “Ninawaombea wagonjwa.” Hakuvutiwa na hilo. Hakutaka mvulana wake afe, mwenye dhambi.

¹⁶³ Nikaingia ndani; walikuwa na lango la kale lenye mpini wa plau wa kufunga ukining’inia juu yake kulifunga (labda wengi wenu watu wa Kaskazini msingejua ni kitu gani), lakini, wa kulifunga lango. Basi nikaingia nyumbani, katika maskini kibanda hicho kidogo, kidogo sana, chenye vyumba viwili (kilionekana kama maskini . . . kile tunachoita “nyumba ya bunduki ya marisau”), kimekaa pale; kuna chumba *hapa*, na hicho ndicho sebule, chumba cha kulala, na yote pamoja; na jiko *kule* nyuma. Nilipoingia . . . Palikuwa ni mahali padogo palipopakwa chokaa, na pazuri, pamepakwa chokaa pande zote, na ubao mwembamba. Kwa hiyo basi . . . La, ninaamini alikuwa na karatasi ya lami juu ya paa, ninakumbuka kuviona hivyo viputo vikubwa, kama vya umande, vikining’inia juu yake.

¹⁶⁴ Ndipo wakati nilipoingia, kulikuwako na alama iliyowekwa pale mlangoni, kasema, “Mungu Bariki Makazi Yetu.” Papa hapa pembeni palikuwapo na kitanda kikuukuu hapa, na kingine hapa. Hapo alilala jamaa mkubwa mno (hakuna zulia sakafuni), mvulana mkubwa mno, kijana mkubwa mwenye sura nzuri amesimama pale. Nadhani alikuwa . . . ana uzito wa ratili mia moja na sabini ama mia moja na themanini, karibu futi sita. Naye alikuwa ameshika blanketi mkononi mwake, akiguna, “Uhum. Uhum.”

¹⁶⁵ Naye akasema, “Kitoto cha mama.”

166 Ndipo nikawazia, “Kitoto cha mama.” Na hata hivyo alikuwa—alikuwa na ugonjwa wa zinaa, kaswende. Naye—naye alikuwa yuafa.

167 Halafu akambusu kwenye paji la uso, na kumpapasa namna hiyo, kasema, “Kitoto cha mama.”

168 Mbona, moyo wangu karibu upasuke. Nikawazia, “Naam, haidhuru umezama jinsi gani katika kilindi cha dhambi, ungali ni kitoto chake.” Ndipo nikawazia, “Mnaona, haijalishi alikuwa katika hali mbaya jinsi gani, angali ni ‘Kitoto cha mama.’” Nikawazia, “Mungu alisema, ‘Mama aweza kumsahau mtoto wake mchanga wa kunyonya; bali kamwe siwezi kukusahau, kwa kuwa jina lako limechorwa katika vitanga vya mkono Wangu.’” Mnaona? Ingewezekanaje!

169 Nikamwangalia maskini huyo mtakatifu kizee akitembea pale. Ungeweza kujua, ndugu, hakuwa na kitu nyumbani; lakini alikuwa na kitu fulani humo nyumbani ambacho kila nyumba Indiana ama kila mahali inapaswa kuwa nacho; hicho ni Mungu. Afadhali niwe na hicho kuliko kuwa na nyumba kubwa nzuri iliyobandikwa picha za wasichana na upuuzi huu wote mchafu, wa kuchukiza. Biblia iliyochakaa imewekwa pale huku imefunguliwa, ina kurasa zilizochakaa na zina makunyanzi.

170 Nikamwangalia. Naye akasema, “Kasisi amekuja kukuombea, kipenzi.”

171 Akahema, “Uhum. Uhum. Giza. Uhum.”

172 Nami nikasema, “Anasema nini?”

Akasema, “Hajui. Daktari anasema, ‘Amerukwa na akili.’” Kasema, “Anafikiri yuko huko kwenye bahari kubwa mahali fulani, naye anavuta mtumbwi makasia, hali amepotea.” Kisha akasema, “Hilo ndilo nisiloweza kuvumilia, Kasisi: kujua mtoto wangu mchanga yuafa, amepotea.” Kisha akasema, “Ninajua ulikuja kunisaidia, maana Bwana tayari ameniambia hivyo.”

Nikasema, “Nitamwombea,” halafu nikasema, “labda Bwana atamponya.”

173 Hilo halikumvutia, alimtaka tu asimame na kusema alikuwa ‘ameokoka.’ Hivyo tu, mradi tu alikuwa ameokoka. Haidhuru, hana budi kuondoka kwa vyovyote vile, kwa hiyo, wakati mmoja; mradi tu ameokoka! Loo, laiti tungaliweza tu kuwa na msimamo kama huo! Yale Makazi ya Milele huko ng’ambo, yeye alijua ataishi pamoja naye tena basi.

Kasema, “Laiti ningalimsikia akisema alikuwa ‘ameokoka.’”

Nikasema, “Na tuiname.” Basi akapiga magoti. Nami nikaishika tu miguu yake, nayo miguu yake ilikuwa baridi sana na inanata. Nami nisingeweza kuifunika, alikuwa amemfunika kwa blanketi ndo—ndogo pale; naye alikuwa ameavaa kaptura zake pekee, mwajua.

174 Na kwa hiyo yeye. . . Naye alikuwa tu akiivuta hiyo nyuma namna hiyo, akifikiria tu alikuwa ndani yake. Akaiishika hiyo kwa nguvu, akifikiri alikuwa akivuta makasia. Akaendelea kusema, “Kuna giza sana. Uhum. Uhum. Kuna giza sana.” Kwa hiyo akajaribu kuzungumza naye; naye anashika tu kusema, “Kuna giza na ni baridi,” akivuta tu.

175 Ndipo ni—nikamwanguka kidogo, naye akapiga magoti pale, ndipo nikasema, “Shangazi, waweza kutuongoza katika maombi?”

Akasema, “Naam, bwana.”

176 Yeye tu, pamoja nami, na huyo mvulana, na Roho Mtakatifu humo chumbani, hao tu. Maskini mtakatifu huyo akaomba. Jamani! Wakati aliposema Naye, ulijua alikuwa amesema Naye hapo awali. Naam, bwana! Alijua yule aliyekuwa akisema naye. Akasema, “Bwana, sijui utakalofanya,” akasema, “bali kila kitu ni kama tu ulivyosema Wewe.”

177 Loo, jamani! Loo! Nina furaha sana, nina furaha sana Yeye angali ni Yesu yule yule kule nyuma pamoja na watakatifu hao kule. Angali ni Yesu yule yule leo.

178 Na kamwe sikumwuliza juu ya dini yake, kama alikuwa ni Mbaptisti, Mpentekoste, ama nini. Hiyo haikuwa kazi yangu. Nilikuwa—nilikuwa tu nikimfuata Roho Mtakatifu, naye alikuwa akifanya jambo lile lile. Tilitaka kuona kile Yeye atafanya.

179 Kwa hiyo tukapiga magoti, naye akaanza kuomba. Alipomaliza kuomba, alisimama na kubusu kichwa cha mvulana huyo, kasema, “Mungu, kibariki kitoto changu.”

180 Ndipo akasema, “Sasa utaomba, Kasisi?”

181 Nami nikasema, “Naam, mama.” Na papo hapo ilikuwa yapata saa mbili u nusu, labda saa tatu kasorobo, nami nilikuwa katika. . . maili mbili kutoka mahali pale, na—nayo ile ndege ikiondoka saa moja; wala sikujua wakati nitakaotoka.

182 Kwa hiyo nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake, nikasema, “Baba wa Mbinguni, sielewi jambo hili. Na Wewe. . . Ni—nilikusudiwa kupanda ndege muda kidogo uliopita, karibu saa moja na nusu iliyopita. Uliendelea tu kusema, ‘Endelea kutembea,’ na hili ndilo jambo pekee ambalo nimepata bado. Naye alisema ya kwamba Wewe. . . aliniona nikija. Kama huyo—kama huyo ni Wewe, Bwana, basi sijui la kufanya ila kuweka tu mikono yangu juu ya mvulana huyu.”

183 Akasema, “Loo, mama,” kasema, “mwangaza unaingia humu sasa.” Na yapata dakika tano kutoka wakati huo, alikuwa ameketi kando ya kitanda, huku amemkumbatia mama yake.

184 Nikaponyoka nikatoka, nikakimbia kule nikachukua teksi, nikakimbia hotelini kuchukua mkoba wangu. Basi nilifikiri ningeenda kule na kungojea tu, labda ingenibidi kungojea siku

moja ama mbili kwenye siku hizo. Mnajua jinsi ilivyokuwa vigumu mara tu baada ya vile vita kule kupata ndege, kwa hiyo nikawazia, “Itanibidi kungojea siku kadhaa.”

¹⁸⁵ Basi nikaingia kwenye teksi na kukimbia huko, kwenye uwanja wa ndege. Nilipokuwa tu nikifika kule, wao wakasema, “Ndege namba 196 ya kwenda Louisville, Kentucky, sasa inaondoka.” Mungu aliishikilia ndege hiyo ardhini kwa ajili yangu, namna hiyo. Loo, ninaamini hilo!

¹⁸⁶ Yapata miaka miwili baadaye, nilikuwa nikishuka kwenda huko kwenye garimoshi, nikienda Arizona, kwa Ndugu Sharrit, kule kwa ajili ya mkutano. Na kwa hiyo nilikuwa nimchukue Ndugu Moore na hao wengine. Na kwa hiyo nilipoenda huko, nilisimama kule Memphis. Ndipo garimoshi likaingia, kama nyote mnajua jinsi linavyoingia likienda magharibi namna hii, ndipo linarudi na kuingia kwenye jukwaa la kugeukia kisha linazimwa.

¹⁸⁷ Nazo hizo sandiwichi kwenye garimoshi, wanaziua kama senti sitini kila moja. Nami ninaweza kuzinunua kwa senti kumi, kumi na tano, mwajua, huko nje mahali pengine. Na kwa hiyo nikangoja mpaka garimoshi liliposimama, nikanunue sandiwichi. Nilikuwa ninaenda kujinunulia ha-... kifurushi kilichojaa hambaga, nipate kuwa na yubile halisi nikienda kule. Kwa hiyo nikaruka nje na kukimbia kupitia kule upesi sana, kwenda kwenye kibanda cha hambaga; nikiwa mwangalifu, litasimama pale kama dakika thelathini.

¹⁸⁸ Na kwa hiyo ni—nikaanza kununua hambaga, ndipo nikasikia mtu fulani akisema, “Halo, hapo, Kasisi!” Basi nikageuka, kofia ndogo nyekundu, amesimama pale akipepesa macho yake, mwajua, kasema, “Hunijui mimi, sivyo?”

“Siamini ninakujua, mwanangu.”

Njoo huku, kasema, “Niangelie vizuri!”

Nami nikasema, “Naam?” Nikasema, “Siamini ninakujua.”

Akasema, “Mimi ninakujua!” Kasema, “Wewe ni Kasisi Branham!”

Nami nikasema, “Naam, hiyo ni kweli.” Nikasema, “Umewahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu?”

Kasema, “La, bwana!” Kasema, “Unakumbuka ile asubuhi ambayo ulishuka ukaja nyumbani na mama yangu alikuwa a-...?”

“Loo!” Nikasema, “Wewe siwe!”

Kasema, “Naam, ni mimi! Naam, ndimi!” Akasema, “Kasisi,” kasema, “Mimi nimepona, mzima, na mwenye afya. Isitoshe, bali mie ni Mkristo sasa!”

¹⁸⁹ Mungu asifiwe! Loo!

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
 juu,
 Wote wakiomba katika Jina Lake,
 Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
 Na nguvu za utumishi zikaja;
 Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
 Atakufanyia vile vile, (Hivi huna furaha?)
 Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao, Haleluya!
 Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Hawana elimu kubwa na kadhalika:

Hivyo basi watu hawa huenda wasijifunze
 kuwa,
 Wala kujivunia sifa za ulimwengu,
 Wote wamepokea Pentekoste yao,
 Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
 Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na kwa
 upana,
 Nguvu Zake zingali ni zile zile,
 Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao, Haleluya!
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Njoo, ndugu yangu, tafuta baraka hii
 Ambayo itaisafisha moyo wako kutokana na
 dhambi,
 Itafanya kengele za shangwe zianze kulia
 Na itaendelea kuiwasha moto nafsi yako;
 Loo, unawaka sasa moyoni mwangu,
 Loo, utukufu kwa Jina Lake,
 Nina furaha sana kwamba mimi . . .

Sasa peana mkono na mtu fulani mbele yako, nyuma, na
 karibu nawe:

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao, Haleluya!

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana...? . . .
. . . mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao, Haleluya!
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

¹⁹⁰ Dini hii ya zamani za kale ni nini? Iianza *hapa* nyuma, nayo inadondoka Damu ya Yesu Kristo kote kote. Loo, jamani! Loo, jinsi nilivyo na furaha kwa ajili ya Injili! Loo! Loo, naam, bwana!

Inadondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi (wafia imani, kote kote)
walioifia ile Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Sasa, ni Injili ya namna gani? Kama ilivyoanza huko Pentekoste, mnaona.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa
Roho Mtakatifu,
Alikuwa ni Yohana Mbatizaji (Mnaona,
alipokea, tumboni mwa mama yake,
mwajua). . . alikufa kama mwanamume;
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,
Yeye alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa
watu kutoka dhambini.

Iliendelea kudondoka damu, naam,
kudondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya ile
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Usingeweza kuiundia dhehebu! Huh-uh!

Kulikuweko na Petro na Paulo, na Yohana
mtakatifu,
Waliyatao maisha yao kusudi Injili hii ipate
kuangaza;

Walichanganya damu yao, pamoja na manabii
wa kale,

Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate
kuhubiriwa kwa uaminifu.

Ikaendelea kudondoka damu, naam,
inadondoka damu,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya ile
Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu iliendelea
kudondoka damu.

Kulikuwako na nafsi chini ya madhabahu,
wakilia, “Hata lini?”

Bwana apate kuwaadhibu wale waliofanya
makosa;

Bali kutakuwako na wengine watakaoitoa
damu ya maisha yao

Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na
mafuriko yake mekundu sana.

Inaendelea kudondoka damu, naam,
inadondoka damu,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya ile
Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

¹⁹¹ Sasa, kuanzia wakati wa Pentekoste, na wafia imani wa Pentekoste, huko chini katika kanisa la Efeso, kuingia katika Pergamo, kuingia katika Thiatira, na huko katika—katika Sardi, katika Efeso . . . ama Filadelfia, na kuendelea mpaka Laodikia. Na sasa kile sisi . . . kilichotukia hapa chini? Kama Biblia ilivyosema, kila kitu kiliingia, na mnyama huyu angeinuka katika Marekani.

¹⁹² Je, mnakumbuka lile ono lililosomwa hapa, 1933? Nilikuwa nikienda . . . Kanisa hili hata halikuwa limejengwa. Sikujua ono ni kitu gani, nililiita “nusu usingizi.” Nilikuwa tu Mhubiri kijana wa Kibaptisti, nasi tulikuwa . . .

¹⁹³ Maisha yangu yote niliona hayo maono, nami nitamwuliza mtu yeyote asimame na kusema kama moja la hayo liliwahi kukosea. La, kamwe halikukosea! Haliwezi! Mnaona? Halitakosea!

¹⁹⁴ Na sasa, na nilipoanza shule ya Jumapili niliingia katika nusu usingizi. Tulikuwa nayo hapa kwenye ile nyumba ya kale ya Masoni, nyumbani mwa Charlie Kern, kundi dogo letu. Nami nikamwona huyu Rais Roosevelt akiuongoza ulimwengu kwenye vita vya dunia. Nikabashiri! Nikasema, “Na kuna itikadi tatu: Nazi, na Ufashisti, na Ukomunisti.” Nikasema . . . (Ni wangapi humu ndani wanaokumbuka?) Nikasema, “Utazameni

Ukomunisti, zote zitaishia mle.” Nikasema, “Ethiopia, Mussolini atakwenda Ethiopia, lakini atashindwa.” Kisha nikasema, “Hatimaye tutaingia vitani na Ujerumani, lakini” nikasema “Ujerumani itajenga ngome, katika zege kubwa mno.” Miaka kumi na mmoja kabla ile Ngome ya Maginoti haijajengwa, miaka kumi na mmoja.

¹⁹⁵ Nikasema, “Kisha baada ya vita... Hatimaye tutashinda. Na baada ya vita kwisha, itakuwa kwamba sayansi itakuwa ikibuni vitu vikuu.” Halafu nikasema, “Watakapovibuni, wataunda gari, nayo magari yataendelea kubadilika umbo.” (Mnajua jinsi yalivyoonekana mwaka wa ’33.) Sasa basi, kasema, “Yatakuwa kama mayai, yatafanana na mayai. Kwa kuwa niliona kwenye barabara kuu, barabara kubwa sana, gari likiteremka barabarani ambalo halikuwa na usukani wowote ndani yake. Lilidhibitiwa na nguvu fulani.” Wanalo sasa hivi.

¹⁹⁶ Nikasema, “Kwenye wakati huo... Sasa wanawaruhusu wanawake kupiga kura; nao wanawake, katika kupiga kura, hatimaye...” Nikasema, “Taifa hili ni taifa la mwanamke, limetiwa alama na mwanamke. Ni mwanamke kotekote katika unabii, kila mahali; na namba kumi na tatu kila mahali katika unabii.” Kisha nikasema, “Ni nchi ya mwanamke, ana uhuru wake hapa. Naye ataliangamiza, yeye ndiye uharibifu wa ulimwengu.”

¹⁹⁷ (Na, Roy, nina barua zako juu ya hilo, yule mwanamke mashuhuri ambaye... “Kila kesi ya jinai... Tumeninii... Nililichunguza sana sasa kufikia ambapo: kila kesi ya jinai iliyopata kufanywa katika Marekani hii, mwanamke alikuwa nyuma yake.” Hiyo ni kweli kabisa. Hao ni wanawake wenye sifa mbaya, mnaona, na kadhalika.)

¹⁹⁸ Sasa, kwa hiyo basi nikasema, “Kutakuwako wakati huo, mnamo wakati huo wanawake wataruhusiwa kupiga kura, nao watamchagua mtu asiyefaa.” Walifanya hivyo katika uchaguzi huu uliopita. Hiyo ni kweli. “Ambao utaaanzisha hiyo ngome. Katika wakati huo itakuwa kwamba—kwamba atatokea mwanamke mashuhuri atakayeinuka Marekani, atavalia mavazi mazuri,” nami nimeandika katika mabano: “(huenda ikawa ni kanisa Katoliki).” Mnaona? “Huyo atachukua uongozi juu ya mamlaka, awashinde wengine Marekani. Atakuwa ni mrembo kwa kuonekana, ila atakuwa na moyo katili sana awezavyo kuwa.”

¹⁹⁹ Nikasema, “Kisha nikaangalia tena, nami nikaona Marekani imelipuliwa tu vipande-vipande. Hapakuwapo na kitu kilichosalia juu yake.”

²⁰⁰ Nami nikatabiri basi. “Sasa hili, hilo lilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI.”

²⁰¹ Basi wazieni! Matano kati ya hayo mambo saba yaliyobashiriwa, yametimia tayari.

202 Kanisa kuchukua mamlaka, kanisa Katoliki. Na kule kuja kwa wakati wa mwisho.

203 Nami nikasema, “Niliona, ilionekana kana kwamba kulikuwako na visiki vikiteketea; miamba, imelipuliwa; nayo Marekani nzima ilionekana tu ukiwa, imekaa hivyo, kadri nilivyoweza kuona mahali nilipokuwa nimesimama.”

204 Nami nikasema, “Ninabashiri, kulingana na vile wakati unavyosonga mbele, itakuwa ni kati ya mwaka huu wa ’33 na wa ’77.” Nayo itabidi ifinywe kwa nguvu sana ipate kupitia hapo.

205 Nasi tumeketi juu ya kipipa cha baruti, enyi marafiki. Kila kitu kiko tayari.

206 Loo, lakini Baba yetu mpendwa wa Mbinguni Yule aliyeahidi, Yule aliyeahidi! Si ni vizuri sana kuwa mtumishi wa Kristo? Mambo yote aliyoahidi! Hebu wazienu; tuna majaliwa. Yeye anaishi papa hapa. Yeye papa hapa pamoja nasi sasa, anajua kila siri ya kila moyo, anajua yote kukuhusu; mioto hiyo inayowaka ikipitia moyoni mwetu, anajua yote kutuhusu, anatupenda.

207 Hivi huna furaha kuwa katika kundi hilo la uchache, usiku wa leo, linaloidumisha ile Imani? Kwa kuwa ilikuwa ni amri Yake, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba Yenu ameona vema kuwapa Ufalme. Na isipokuwa kazi hii ifupishwe, kusingekuwako na mtu yeyote mwenye mwili angeokolewa.” Mnaona, tuko moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho.

208 Wapentekoste wakiwa baridi, vuguvugu, wametapikwa kutoka katika kinywa cha Mungu.

209 Ni kundi dogo kabisa lililotolewa hapa nje, wachache tu, lakini kutokana na hao itakuja: “Tazama, Bwana-arusi yuaja!” Na itakapotokea, kila moja ya hizo zamu, kila zamu ya hizi zamu, kuninii. . . Kumbukeni, kuna zamu saba zake. Nasi tuko moja kwa moja katika zamu *hii* ya mwisho. Lakini kila mmoja wa hao wanawali huko nyuma kupitia *hapa* aliamka. Amina! Loo, ilikuwa ni kitu gani? Roho Mtakatifu yule yule.

210 Ndipo kanisa likiisha kuondoka katika. . . Kama tulivyolichukua Jumapili usiku, Yusufu kujitambulisha kwa Israeli, ndugu zake, alimwondosha bibi-arusi wake, kila kitu, na kuwarudisha kwenye ikulu. Ndipo akasimama peke yake pamoja na Wayahudi, na kusema, “Mimi ni Yusufu, ndugu yenu.”

211 Liweke moja kwa moja kwenye Maandiko ambapo walisema wangetenga siku ya maombolezo, na kila nyumba ikiomboleza peke yake.

212 Wao wakasema, “Ulipata wapi makovu haya?”

Kasema, “Mikononi mwa. . .”

“Mikononi mwako?”

Kasema, “Katika nyumba ya marafiki Zangu.”

213 “Wale waliomchoma watamwanguka.” Naye Yule pale amesimama, yule Yusufu.

214 Yeye alisema, “Msininii...” Kama Yusufu alivyosema, “Msijikasirikie, maana Mungu alifanya hivyo kuhifadhi maisha.” Kitu gani? Maisha ya Kanisa, Mataifa, “Kwa ajili ya Jina Lake, watu kutoka kwa Mataifa.”

215 Loo, tuko mwisho, ndugu zangu. Tumewasili! Jina la Bwana libarikiwe! Hebu tuuimbe wimbo huu mzuri wa kale, kama ndugu na dada wapentekoste, pamoja. Sasa, mnasema, “Vema, mimi ni Mbaptisti.” Lakini kama una Baraka za Kipentekoste, wewe ni mpentekoste. Uh-hum. Vema. Vema:

Kibarikiwe kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko juu.

216 Sasa sikilizeni, enyi marafiki. Kama akiwepo mtu hapa miongoni mwetu, ambaye kama mahali popote katika safari ya maisha, ambapo chuki kidogo imeingia moyoni mwako, (Nisikilizeni mimi!) iondoe humo sasa. Ondoa hiyo, kamwe usiruhusu kitu chochote. . .

[Dada mmoja ananena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mmoja anatoa ujumbe—Mh.]

Amina.

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine kisha anafasiri—Mh.]

Amina. Amina.

217 Bwana Yesu, tunakushukuru kwa ajili ya jumbe hizi. Zinatuchangamsha, Bwana tukijua ya kwamba hatujaiacha imani bali tumeishika. Loo, ninaomba, Mungu, ya kwamba Roho ataendelea kukaa kanisani. Tuweke karibu sisi kwa sisi, Baba. Tuweke pamoja na Wewe. Na utembe miongoni mwetu, Bwana, katika wakati huu wa mwisho wa kinara cha taa tunamoishi ndani yake. Kuwa Nuru yetu. Tuangazie, nyakati hizi kuu za giza, Bwana, kwa kuwa tunatambua ya kwamba *kinara cha taa* na *nyota* zinanena juu ya “giza.” Pia Bwana, tuna furaha ya kwamba sisi ni watoto wa Nuru, tunaotembea katika Nuru ya Mungu. Hatujanaswa na mambo haya ya duniani, bali sisi ni watoto Wako. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya mambo haya.

218 Tunakushukuru Wewe kwa sababu ya kutuma jumbe hizi kama thibitisho la Neno Lako. Daima na uheshimiwe miongoni mwetu, Baba. Naomba utuweke mbali na chuki yote ya duniani. Tuweke tumetakaswa, kusudi maisha yetu yawe safi na yaliyotakaswa na matakatifu mbele Zako. Jalia Damu ya Yesu Kristo ifanye hivi kwa kila mmoja wetu, Bwana. Ondoa

miongoni mwetu, kama kuna chochote kamwe ambacho si sahihi. Tuondolee, Bwana. Huu ni wakati wa kuchunguza.

²¹⁹ Mikutano hii imekusudiwa kwa kusudi hilo kuichunguza mioyo yetu. Ulisema hiyo miali ya moto machoni Mwako, “hutafuta na kujua makusudi ya moyo.” Hakika unajua, Baba. Nawe nena nasi tena huku ukitwambia kufanya... kujiweka tayari kwa ajili ya ile saa inayowadia.

²²⁰ Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya hili, Baba. Tutafanya hivyo kwa yote yaliyo ndani yetu kwa neema Yako. Amina.

²²¹ Loo, hivi hamumpendi? Sasa, kama kuna mgeni kati yetu, hivyo ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, mtu mmoja alimwuliza kuhusu kisa cha ndoa na talaka ama kitu fulani, akasema, “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.” Hatuna budi kurudi huko mwanzo.

²²² Basi kama hapo mwanzo lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste, Naye ni Mzabibu, sisi ni matawi, kila wakati Mzabibu huo unapozaa kanisa, litakuwa ni kanisa la Kipentekoste, tawi la Kipentekoste; kitu kile kile lilichokuwa hapo mwanzo (Mnaona?), kila wakati. Sasa, unaweza kupandikiza mizabibu mingine ndani yake na itazaa matunda yake. Unaweza kuchukua m—mchungwa na kupandikiza limau juu yake, litazaa malimau likiishi kwa uhai wa mchungwa huo. Pandikiza mbalungi kwake, nao utazaa balungi maana ni tunda aina ya chungwa.

²²³ Kwa hiyo mashirika haya, madhehebu na kadhalika, yaliyopandikizwa pale, yakijiita Wakristo, wanaweza kuishi kwa uhai wa Kikristo. Hiyo ni kweli kabisa, bali watazaa matunda ya kimadhehebu. Hiyo ni kweli. Maana hawana budi kujipandikiza namna hiyo. Lakini kama tawi hilo lenyewe likiwahi kutoa ninii... ama kama Mzabibu huo ukiwahi kuzaa tawi, litakuwa... litaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Hiyo ni kweli kabisa. Maana hivyo ndivyo ilivyotendeka mara ya kwanza. Kila tawi litakalozaa lenyewe litakuwa na machungwa, kila moja. Nayo Biblia imenena; ilikuwa na matawi kumi na mawili juu yake.

²²⁴ Loo, nina furaha sana kuwa nikiishi chini ya tawi hilo, nanyi je? Naam, bwana. Loo, ni ajabu sana.

²²⁵ Vema, kumbukeni kesho usiku sasa kwenye wakati wa Fila... wa Sardi. Kule...?...kujitokeza kwa dhehebu la Kilutheri, Martin Luther...?...



WAKATI WA KANISA LA THIATIRA SWA60-1208
(The Thyatirean Church Age)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Alhamisi jioni, tarehe 8 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org